epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Mei 17, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581679
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22
**XAVI AELEZA SABABU KUTOMTUMIA ROQUE**

UKURASA WA 3
**DAR YAONGOZA KWA DAWA ZA KULEVYA, BISKUTI ZAKE BADO TISHIO MITAANI**



UKURASA WA 4
**ADAIWA KUMUUA MWANAWE KISA KUJIPAKA KINYESI**

UKURASA WA 5
**KATIBU MKUU WA ZAMANI EAC ACHUNGUZWA**

# Vita uhalifu mtandaoni



• **Timu** ya pamoja; Wizara ya Habari, polisi, mahakama, DPP kunasa wahalifu kidijitali... *Endelea ukurasa 2*





Illustration: Kondo Haruni Kondo, binharun79@gmail.com

## Deni la serikali kwa vyombo vya habari latikisa bungeni

UK.2

UKURASA WA 22

## BAYERN KUMSHAWISHI TUCHEL KUBAKI

BAADA ya kukataliwa na makocha mbalimbali, Bayern Munich imeripotiwa kufikiria upya kuondoka kwa Thomas Tuchel kama kocha na kutafuta suluhu ya...



## NEMC yazipa hospitali miezi mitatu taka zake zitoweke

UKURASA 4

**MICHEZO** GAMONDI: YANGA BADO HAIJAFIKIA MALENGO UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Tulia Ackson, akiongoza Kikao cha kwanza cha Kamati ya kuratibu Maandalizi ya Mkutano wa 6 wa Maspika wa Mabunge Duniani Geneva nchini Uswisi jana. **PICHA: BUNGE**

# Deni la serikali vyombo vya habari latikisa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wamegeuka 'mbogo' bungeni wakiitaka serikali kulipa madeni inayodaiwa na vyombo vya habari kwa kutenga kwenye bajeti.

Wabunge hao wamesema kuendelea kuwapo kwa madeni hayo kunachangia kuvididimiza, hivyo kushindwa kustawi na kushindwa kujiendesha.

Pia wamesema kumekuwa na kauli za kuagiza kulipwa kwa zaidi ya Sh. bilioni 19 za madai hayo, lakini utekelezaji umekuwa wa kusuasua hali ambayo inataka hatua zaidi kuchukuliwa.

Wakichangia jana hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolijia ya Habari kwa mwaka 2024/25, wabunge hao walisema hali ya vyombo vya habari kiuchumi si nzuri hali inayoonyesha hata kwenye kikokotoo kutakuwa na shida kwa kuwa waajiri wanashindwa kupeleka michango ya wanachama kutokana na hali ngumu.

Mbunge wa Singida Magharibi (CCM), Elibariki Kingu, alisema hadi jana vyombo vya habari nchini vilikuwa vinaidai serikali zaidi ya Sh. bilioni 19 na kwamba kwa zaidi ya miaka saba havijalipwa.

"Nape tunasema kwa nia njema lazima serikali mje na mikakati. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2017 na George Ogalo kuhusu Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) vyombo vya habari vinategemea asilimia 80 hadi 85 ya matumizi ya serikali. Hauwezi kuepuka 'government expenditure' (matumizi ya serikali) katika kukuza uhuru wa vyombo vya habari nchini na kuvisaidia," alisema.

Kingu alitaka serikali kukaa na Wizara ya Fedha kuvilipa vyombo vya habari fedha zinazoidai ili vijiendeshe, hivyo kukuza ajira mitaani.

"Hizi fedha Sh. bilioni 19 haziko katika mzunguko kwa vyombo vya Habari. Hivi tunategemea vyombo vya habari vifichuaje maovu kama vinadai fedha? Haviwezi kuwalipa watumishi wao mishahara. Kaeni na Wizara ya Fedha kuhakikisha vyombo hivyo vinalipwa ili kuhamasisha utendaji na kukuza sekta ya habari katika taifa," alisema.

Alisema alichukua takwimu kutoka nchi ya Kenya na kubaini kuwa asilimia 30 ya mapato ya magazeti yanatokana na matumizi ya serikali na kumtaka waziri kuwasaidia wanahabari watanzania ili kuacha alama nchini.

"Nashauri serikali itenge angalau kwa asilimia fulani ya matumizi ya serikali kwa ajili ya vyombo vya habari, hakuna namna ambayo mnaweza kukuza vyombo vya habari kama mtawaacha wahangaike wenyewe, kuanzia leo nabeba ajenda ya kuwa msemaji wao serikali ilipe madeni ya vyombo vya habari,"alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Ester Bulaya alipendekeza angalau katika bajeti kuu serikali kutenga angalau asilimia 0.3 ya bajeti kwa ajili ya kulipa kwa madeni hayo na kwamba hiyo itawafanya kulipa kwa wakati na kwa bei ya soko ya matangazo ya vyombo vya habari nchini.

"Vyombo vya habari hutegemea matangazo kutoka serikalini vitu vingine ni vya ziada, wanapolipwa ndio wataweza kulipa mishahara, kujiendesha na kufanya mambo mengine, leo wana madeni sugu zaidi ya Sh. bilioni 18 na bado kuna vyombo vingine havijaorodheshwa," alisema.

Alisisitiza katika suala la kikokotoo, waandishi wa habari watakuwa na hali ngumu kwa kuwa hata michango yao haipelekwe ipasavyo katika mfuko ya hifadhi ya jamii.

Naye Mbunge wa Buchosa (CCM), Erick Shigongo, alisema kuna hali mbaya katika vyombo vya habari hivi sasa ambapo wafanyakazi wanashindwa kulipwa mishahara.

"Kuna hali ngumu sana, labda kama mmeamua kwamba acha vyombo vya habari vife ili tufanye mambo yetu sawasawa. Hakuna maendeleo bila vyombo vya habari. Ninachoomba kila wizara katika nchi hii ina kitengo cha Habari, naomba kila bajeti ya wizara angalau iwe inatengwa angalau asilimia moja ya bajeti iende kwenye idara ya habari,"alisema.

Alisema asilimia moja hiyo mwisho wa siku itaishia katika vyombo vya habari ambapo watalipana mishahara na kuwa ruzuku ya serikali ikienda katika vyombo vya habari watawafunga mdomo.

"Sisi vyombo vya habari hatuhitaji ruzuku ya serikali, Ruzuku ya serikali ikija kwetu mtatufunga mdomo. Turuhusuni tufanye biashara na serikali na vyombo vya habari vya serikali vijitoe kwenye matangazo. Haiwezekani ITV wapambanie matangazo na TBC si sahihi.

"BBC ya Uingereza haichukui matangazo kwa sababu ina ruzuku ya serikali. TBC wanapata ruzuku waache kushindana na vyombo binafsi na tukifanya hivi nina uhakika kuwa vyombo vya habari binafsi vitakuwa na nguvu," alisema.

Akijibu hoja za wabunge, Nnauye alisema serikali itahakikisha madeni yanayodaiwa na vyombo vya habari kwa taasisi za serikali yanalipwa.

Aidha, alisema vyombo hivyo viko salama chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan na kwamba atakuwa mkali hasa kwa taasisi ambazo zinadhani huduma zinazopewa na vyombo vya habari ni za bure.

Alisema fedha ambazo baadhi ya vyombo vya habari inazidai taasisi za serikali zilitengwa hata hivyo hawakulipa.

"Nakubaliana na nyie wabunge na nadhani kuna haja ya kuwa wakali kidogo hasa kwa taasisi ambazo zinaona kama hizi huduma ni za bure. Kuna watu wanafanya kazi, kuna watu wanatoka jasho, kuna vifaa vinatumika, kuna uwekezaji umefanyika , kuna kodi tunalipa kutowalipa ni uharamia ambao hatuwezi kukubali," alisema.

# Vita uhalifu mtandaoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UHALIFU wa mtandaoni unaoripotiwa katika maeneo mbalimbali nchini, serikali imeweka mkakati kuutokomeza.

Mkakati huo unahusisha timu ya pamoja inayoundwa na taasisi za serikali, ikiwamo Wizara ya Habari, Jeshi la Polisi na mahakama kuwashughulikia wahalifu kwa mbinu za kidigiti.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye alibainisha hayo bungeni jijini hapa jana, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/25.

Bunge jana liliidhinisha makadirio hayo, Sh. bilioni 180.92 zikitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi tisa inayolenga kuimarisha utoaji huduma za uhakika na za gharama nafuu za habari, kuweka mazingira yanayokuza ubunifu katika kubadilisha Tanzania kuwa na uchumi wa kidijiti.

Waziri Nape alisema fedha hizo zitatumika kutekeleza mipango mbalimbali ikiwamo kujenga maabara za akili mnemba (AI) na matumizi ya roboti nchini.

Alisema kwa mwaka ujao wa fedha, pia wamepanga kujenga mfumo wa kufungamanisha taarifa za kila mwananchi ili kuwa na akaunti ya kidijiti itakayomwezesha kutumia huduma mbalimbali za kidijiti nchini.

### SHERIA YA TEHAMA

Waziri Nape alisema wizara imepanga kuratibu maandalizi ya Sheria ya TEHAMA itakayojumuisha maeneo ya Teknolojia zinazoibukia ikiwamo teknolojia ya akili mnemba (AI).

Alisema wataanzisha kituo kimoja cha usalama wa mawasiliano cha taifa; kuhuisha mfumo wa takwimu za makosa na matukio ya mtandao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na mahakama; kuongeza uwezo wa Kitengo cha Uchunguzi wa Kidijiti kwa Jeshi la Polisi katika ofisi ya makao makuu ya Dar es Salaam na Kanda ya Zanzibar.

Pamoja na hayo, Waziri Nape alisema wamepanga kuratibu mapitio ya Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015, kuandaa viwango vya matumizi ya TEHAMA Tanzania, kuboresha mfumo wa kutambua na kusajili wataalamu wa TEHAMA nchini na kuendelea kufanya utafiti kuhusu mwelekeo wa maendeleo ya TEHAMA nchini.

"Pia kuwezesha ujenzi wa Vyuo vya TEHAMA Nala - Dodoma na Buhigwe - Kigoma; kukamilisha usakinishaji, uanzishwaji na matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (Jamii Data Lake) nchini; kuendelea na utekelezaji wa Programu za Anga la Juu ikiwamo kuratibu uanzishaji wa Wakala ya Anga la Juu nchini (Tanzania Space Agency) kwa ajili ya kukuza matumizi ya teknolojia za Setelaiti katika kuwezesha urahisi na unafuu katika upatikanaji huduma za mawasiliano na huduma nyingine ikiwamo ulinzi na usalama, utafiti na kukabiliana na majanga na utabiri wa hali ya hewa nchini," alisema.

Waziri huyo pia alisema wamepanga kuanzisha programu maalum ya TEHAMA kwa vijana kwa lengo la kukuza ujuzi wa TEHAMA nchini katika ngazi zote.

Vilevile, alisema Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA) imepanga kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano nchini na kukamilisha na kusimamia uanzishwaji wa Bodi ya Ithibati, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Wanahabari na kuhuisha muundo wa maofisa habari serikalini.

### MIKOA SITA

Waziri Nape pia alitaja mikoa sita iliyoripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio ya wizi wa kimtandao ambayo ni Rukwa, Morogoro, Dar es Salaam, Tabora, Songwe na Mwanza.

Pia akasema kuwa takwimu zinaonesha laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 62.3 Aprili, 2023 hadi laini milioni 72.5 Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 16.4.

Alieleza kuwa watumiaji intaneti wameongezeka kutoka milioni 33.1 Aprili, 2023 hadi milioni 36.8 Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 11.2.

"Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea fedha kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka milioni 44.3 Aprili, 2023 hadi milioni 53 Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 19.6," alisema.

# Dar yaongoza matumizi dawa za kulevya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKOA wa Dar es Salaam umetajwa kuwa unaongoza kwa kukamatwa dawa za kulevya na kwamba maeneo makubwa ya starehe (klabu) na fukwe hutumika kuuza biskuti za bangi.

Kutokana na hali hiyo, WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, amesema serikali imejipanga kutupia jicho la ziada kudhibiti matumizi na biashara ya dawa hizo.

Akitoa taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2023, Waziri Mhagama alisema idadi kubwa ya watumiaji wa dawa za kulevya nchini ni vijana kwa wastani wa asilimia 78, hali inayoathiri nguvu kazi ya Taifa.

"Mkoa unaoongoza hadi sasa ni Dar es Salaam. Tutazunguka lakini ukirudi Dar es Salaam unakutana nao. Tunashukuru sana Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imejipanga vizuri na imefanya kazi nzuri sana. Tutazunguka nchi nzima lakini kwa Dar es Salaam tumeweka kituo.

"Hadi kufikia Desemba 2023, waraibu 903,062 wa dawa za kulevya na vilevi vingine walipatiwa huduma katika hospitali hizo. Hii ni hatua muhimu katika kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile, uraibu, UKIMWI, kifua kikuu, homa ya ini, magonjwa ya akili na yasiyoambukiza," alisema.

Kwa kipindi hicho, alisema mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, ilikamata kilogramu 1,965,340.52 zikihusisha watuhumiwa 10,522 (wanaume 9,701 na wanawake 821).

"Dawa zilizokamatwa ni heroin kilogramu 1,314.28, cocaine kilogramu 3.04, methamphetamine kilogramu 2,410.82, bangi kilogramu 1,758,453.58, mirungi kilogramu 202,737.51, skanka kilogramu 423.54 na dawa tiba zenye asili ya kulevya gramu 1,956.9 na mililita 61,672," alisema.

Pia alisema dawa hizo zilizokamatwa ni karibu mara tatu ya kiasi kilichokamatwa kuanzia mwaka 2012 hadi 2022, ambacho ni kilogramu 660,465.4.

Mhagama alisema dawa ngeni zilizoanza kuingizwa nchini hivi karibuni kama vile methamphetamine, skanka na biskuti zilizochanganywa na bangi pia zilikamatwa katika kipindi hicho.



Katika kuongeza mapambano dhidi ya dawa za kulevya, alisema serikali imetunga Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024 inayolenga mambo mbalimbali ikiwamo kuimarisha udhibiti wa dawa za kulevya zinazozalishwa nchini kama vile bangi na mirungi.

"Sera inatoa maelekezo ya kufanya utafiti wa mazao mabadala katika maeneo yaliyokithiri kwa kilimo cha mazao hayo ili wananchi wa maeneo husika wajihusishe na kilimo cha mazao halali badala ya kilimo cha bangi na mirungi," alisema.

Pia alisema sera inaelekeza kuwajengea uwezo wadau mbalimbali katika udhibiti wa dawa za kulevya ili ushiriki wao ulete tija katika mapambano hayo

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, alisema zaidi ya kesi 7,000 zimetolewa hukumu na serikali imeshinda kwa asilimia 83 ya kesi zote na asilimia 17 ambazo ilishindwa kwa kukosa ushahidi.

Kuhusu biskuti za bangi, Kamishna wa Kinga na Tiba wa DCEA, Dk. Peter Mfisi, alisema bei yake ni kubwa kuliko iliyotengenezwa na unga na zinauzwa kwenye klabu kubwa na fukwe.

"Mtu akinunua si kwamba amenunua kwa bahati mbaya wanataka kuwafundisha na watoto wetu ambao wazazi wana uwezo wa kuwapa Sh.1,000 kwenda nao shuleni ndio wanaolengwa sana. Wale ambao hawazijui wanapewa kama kuwafundisha ili watumie," alisema.

Alisema biskuti hizo zilizotengenezwa kwa bangi hazina lebo na hazina shepu nzuri kama zingine na wanaonunua wanajua.

"Tunaendelea kutoa elimu kwa jamii unapokuta biskuti lazima usome, zimetengenezwa wapi, vitu vilivyotumika ukiona mtu amekuletea au hazina shepu utaingizwa kwenye utumiaji huo, ili ukizoea uendelee kutumia kila siku,"alisema.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende **"pay via mobile"**. Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-6



Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# NEMC yazipa miezi mitatu hospitali taka zake zitoweke

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI na zahanati zimepewa siku 90 kutafuta makandarasi wenye sifa za kuzoa taka hatarishi zinazoweza kusabisha athari kwa afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira.

Agizo hilo lilitolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji Sheria wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Hamad Kisiwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

NEMC imetaja taka hatarishi kuwa ni zinazotokana na huduma za afya kama za dawa zilizotumika, zenye mgando wa damu na sehemu za mwili wa binadamu zilizoondolewa kwa zababu za magonjwa mbalimbali.

Imetaja taka zingine kuwa ni zenye viambukizi vya magonjwa, vitu vyenye ncha kali (sindano, nyembe), dawa na taka zenye mionzi.

Alisema baada ya siku hizo 90, NEMC itaanza kufanya ukaguzi kwenye hospitali hizo na ambao hawatakuwa na wakandarasi wenye sifa za kuzoa taka hizo watachukuliwa hatua za kisheria.

Kisiwa alisema Wizara ya Afya ina mwongozo wa namna ya kutenganisha taka hizo kwa kutumia rangi tofauti kulingana na kiwango cha uhatarishi.

Alisema taka hatarishi zinazotokana na huduma za afya zinaweza kusababisha milipuko ya magonjwa na vifo iwapo taratibu za ukusanyaji, utunzaji na uteketezaji wa taka hizo hautazingatiwa.

Hivi karibuni, Kisiwa alisema kumekuwepo na taarifa na kushuhudiwa kwa ukusanyaji, usafirishaji na utupaji holela wa taka zinazotokana na huduma za afya katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema mwaka 2023, Baraza lilipata taarifa ya uwepo wa kiwanda kinachorejeleza taka zitokanazo na huduma ya afya maeneo ya Kigamboni na Baraza lilishuhudia ukiukwaji mkubwa wa sheria kwa kuwa taka hizo nyingine zilikutwa zikiwa bado na majimaji na damu mbichi.

Kwa mujibu wa Kisiwa, kiwanda hicho kilisitishiwa huduma yake na kutozwa faini ili kujirekebisha.

Alisema mwezi huu, baraza lilipewa taarifa ya utupaji holela wa taka za aina hiyo katika maeneo ya Kibaha na kufanya ufuatiliaji na kubaini kadhia hiyo.

Pia alisema vijana wanaofanya usafi maeneo ya fukwe wamekuwa wakikusanya taka zinazotokana na huduma za afya kwenye fukwe na nyinginezo mara kwa mara hali inayohashiria kuwepo kwa utupaji wa taka hizo kiholela kwenye vyanzo vya maji hasa baharini na mitoni.

"Ikumbukwe kuwa usafirishaji na utupaji taka hizo hovyo bila kufuata miongozo na kanuni zilizopo unaweza kuleta athari kubwa kwa mazingira, binadamu pamoja na wanyama ikiwemo kuzuka kwa magonjwa mbalimbali na kusababisha hasara kubwa kwa serikali yetu ambayo itatumia fedha nyingi katika kudhibiti magonjwa na athari hizo," alisema.

Alisema taka zinazotokana na huduma za afya zinajumuisha, taka zenye kuambukiza magonjwa, za kipatholojia, vitu vyenye ncha kali, dawa, genetoksiki, taka zenye mionzi, taka za mgando wa damu na dawa za binadamu.

## Serikali yaahidi kufuatilia mikopo umiza ya bodaboda

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema inafuatilia kwa karibu mikopo inayotolewa kienyeji kwa watu bila kufuata sheria na kanuni na baadaye kugeuka mizigo mikubwa na kuwaumiza wakopeshwaji.

Pia imesema inatambua kundi kubwa linalaumia zaidi ni watoa huduma ya usafiri wa pikipiki, maarufu kama bodaboda. Imesema lengo ni kuwawekea mipaka Watanzania kutoumizana pale wanapoamua kupeana mikopo kwa kusaidiana kwa kuwa kuna baadhi ya watu hutumia shida za wengine kama fursa ya kujinufaisha.

Hayo yalisemwa jana bungeni baada ya Mbunge wa Viti Maalum, Anatropia Theonest, kuhoji kwa nini serikali isitunge sera, kanuni na sheria maalum kuwalinda watoa huduma ya usafiri wa bodaboda na mikopo inayoumiza kutoka kwa wakopeshaji binafsi.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema suala hilo haliko tu kwa madereva wa bodaboda bali watu mbalimbali, kutokana na ujamaa wa kukopeshana bila kufuata misingi ya sheria na kanuni za mikopo.

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

SALAMU ZA PONGEZI



Mr. Emmanuel M. Kilimba
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi

Wajumbe wa Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), tunakupongeza **Bw. Emmanuel Martin Kilimba** kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi.

Tuna Imani kubwa kuwa chini ya Uongozi wako, Bodi yetu itaendelea kusonga mbele kwa mafanikio na kutimiza malengo yake ya uendeshaji wa Benki. Tunaahidi kukupa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yako kwa kuweza kukuza uchumi wa nchi.

TCB Benki inayomuelewa Mtanzania

**HONGERA SANA**

**Tanzania Commercial Bank (TCB)**
Makao Makuu, Jengo la PSSSF,
Barabara ya Bagamoyo, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho,
Kijitonyama, Baruapepe: info@tcbbank.co.tz, callcentre@tcbbank.co.tz

www.tcbbank.co.tz @Tanzaniacommercialbank

# Adaiwa kumuua mwanawe kisa kujipaka kinyesi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MTOTO Alvin Fabian mwenye umri wa miaka mitatu, mkazi wa kijiji na kata ya Malya, Kwimba mkoani hapa, anadaiwa kupigwa hadi kuuawa na baba yake mzazi, Fabian Pauline (32), baada ya kumkuta amejisaidia haja kubwa na kujipaka.

Tukio hilo lilitokea Mei 9, mwaka huu, majira ya saa 4:00 asubuhi baada ya Pauline kumkuta mwanawe katika hali hiyo kisha kuanza kumshambulia kwa kipigo katika maeneo mbalimbali ya mwili hadi kumsababishia kifo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna (DCP) Wilibroad Mutafungwa, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo na kusema mwili wa mtoto huyo tayari umefanyiwa uchunguzi na kukabidhiwa ndugu kwa mazishi.

Alisema mtuhumiwa Pauline anaendelea kushikiliwa na jeshi hilo na kwamba atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Katika hatua nyingine, Mutafungwa alithibitisha kukamatwa kwa Ezron Macheya (47), dereva na mkazi wa Kigungumule wilayani Magu kwa tuhuma za kumpiga kwa ubapa wa panga, fimbo na mkanda wa suruali sehemu mbalimbali za mwili wa mtoto wake wa kike, mwenye umri wa miaka minane na mwanafunzi wa darasa la kwanza (jina la shule linahifadhiwa).

Macheya anadaiwa kumsababishia maumivu makali sehemu za mapaja, mgongoni na mkono wa kulia baada ya kumpiga mtoto huyo kwa madai kuwa amekuwa na tabia ya kuzurura mtaani usiku na kuchelewa kurudi nyumbani.

Kamanda Mutafungwa alisema mtoto huyo amepata michubuko sehemu mbalimbali za mwili wake na alipelekwa kituo cha afya Kisesa kwa ajili ya matibabu na hali yake inaendelea vizuri na kwamba mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa.

**Mtoto huyo amepata michubuko sehemu mbalimbali za mwili wake na alipelekwa kituo cha afya Kisesa kwa ajili ya matibabu na hali yake inaendelea vizuri na kwamba mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa.**

Kamanda Mutafungwa pia alithibitisha kutokea kwa kifo cha mfanyabiashara na mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, Amani Manyama (31) anayedaiwa kujinyonga kutokana na msongo wa mawazo.

Alisema mfanyabiashara huyo Mei 14, mwaka huu, majira ya saa 3:00 asubuhi, alikutwa kukutwa amejinyonga hadi kufa kwa kutumia waya wa kuanikia nguo kwenye mwembe nje ya nyumba ya babu yake, Berson Machumu (67).

Alisema Manyama alikuwa anasumbuliwa na maradhi mbalimbali na kulazwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando Mei 12, mwaka huu, na kuruhusiwa siku iliyofuata baada ya kupata nafuu, hivyo kudaiwa kuwa na msongo wa mawazo juu ya maradhi yaliyokuwa yakimsibu.

# ACT yataka tume kuchunguza mauaji ya raia

**Romana Mallya na Sabato Kasika**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimelitaka Bunge kuunda tume ya kuchunguza mauaji yote ya raia ili kujiridhisha na hatua zilizofanywa na Jeshi la Polisi.

Aidha, chama hicho kimetangaza kutoshiriki uchaguzi wa marudio wa ubunge wa Kwahani, Zanzibar, unaotarajiwa kufanyika Juni 8, mwaka huu, kikitaka Tume Huru ya Uchaguzi ijiuzulu.

Vilevile, wameitaka Tume ya Haki za Binadamu kufanya ukaguzi wa haraka katika Magereza, vituo vya polisi na maeneo mengine ya vizuizi ili kuona hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani wa chama hicho, Dahlia Majid Hassan, aliyasema hayo jana wakati ACT- Wazalendo ikichambua bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Katika uchambuzi huo, Dahlia alisema chama hicho kinaitaka serikali kuhakikisha maofisa wa Jeshi la Polisi wanaotuhumiwa na mauaji kusimamishwa ili kupisha uchunguzi.

Alisema chama hicho kinasikitika kuona chombo cha usalama wanachokitegemea kwa ajili ya kulinda usalama na amani ya wananchi, kimekuwa ni moja ya chombo ambacho kinaondoa amani na usalama wa wananchi.

Kuhusu Jeshi la Polisi kutumika kuminya mfumo wa utoaji wa haki, alisema mfumo wa ukamataji bado ni wa kikoloni.

Kutokana na changamoto hizo, Dahlia alisema chama hicho kinaitaka serikali kutenga fedha za kutosha kununua zana za kisasa za uchunguzi na kutenga fedha maalum kwenye Mfuko wa Fedha za Upelelezi ambao uko kisheria, ili kutoa nguvu na uwezo wa upelelezi kufanyika kwa kina.

Pia alisema serikali iwekeze kwenye mafunzo, vifaa vya kisasa ili kubaini viashiria vya uhalifu na kuvizuia kabla kutokea kwa vitendo vyenyewe.

Kadhalika, aliitaka serikali kuachana na polisi kuwa kama waendesha mashtaka katika mahakama.

Kuhusu msongamano wa mahabusu na hali ya usalama katika magereza, alisema chama hicho kinasisitiza matumizi ya adhabu mbadala kama inavyobainishwa katika kifungu 3 (1) cha Sheria: The Community Services Act (Cap. 291 R.E. 2019) ili kupunguza msongamano.

Akizungumzia matukio ya uhalifu dhidi ya wanawake, wazee na watoto, Dahlia alisema chama hicho hakiridhishwi na hatua za serikali katika kukabiliana na uhalifu dhidi ya makundi hayo.

Kuhusu ongezeko la ajali za barabarani, alisema serikali inapaswa kuangalia suala hili kwa ukaribu zaidi ili kuepuka na kupunguza vifo vya watu wanaokufa kutokana na ajali zinazosababishwa na uzembe wa madereva mwendokasi na ijenge barabara kwa kiwango kinachotakiwa.

# Katibu Mkuu wa EAC achunguzwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KAMATI ya Sheria, Haki na Hadhi za Wabunge ya Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) imeanza kufanya uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili aliyekuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), DK. Peter Mathuki.

Dk. Mathuki anakabiliwa na tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka na kusababisha upotevu wa fedha zaidi ya Dola za Marekani milioni sita zilizoibuliwa na Bunge hilo.

Raia huyo wa Kenya hivi karibuni nchi yake ilimwondoa madarakani kutokana na tuhuma hizo na anatarajiwa kuhojiwa na kamati hiyo ili kujibu tuhuma zinazomkabili.

Tuhuma zinazomkabili ni matumizi mabaya ya fedha za Mfuko wa Usalama, uuzwaji mali za jumuiya kwa bei ndogo yakiwamo magari bila kufuata sheria na kuajiri wafanyakazi bila kushirikisha ofisi inayohusika na ajira.

Tuhuma zingine ni kuhamisha wafanyakazi bila kuzingatia utaratibu, kuajiri walinzi bila kufuata utaratibu na kufungua akaunti za fedha bila kufuata utaratibu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika makao makuu ya EAC yaliyoko jijini Arusha, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mashaka Ngole, alisema tuhuma hizo ziliwasilishwa katika Bunge hilo wakati wa kikao kilichofanyika Kenya na kupokewa na Spika wa Bunge hilo na baadaye kuwasilishwa kwenye Kamati ya Bunge.

Dk. Matuki aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa EAC Februari 27, 2021 wakati wa mkutano wa kwanza wa wakuu wa nchi uliofanyika kwa njia ya mtandao.

Dk. Mathuki ambaye hivi karibuni aliteuliwa na nchi yake kuwa Balozi wa Urusi, nafasi yake inashikiliwa na Caroline Mueke, aliyependekezwa hivi karibuni na serikali yake ya Kenya kumalizia kibarua cha miaka miwili iliyosalia.

twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

## UNAUDITED RESULTS FOR THE PERIOD ENDED 31 MARCH 2024

### CHAIRMAN'S STATEMENT

We faced a weak market at the beginning of the year due to heavy rains, projects slow down and export drops. Despite these challenges, March has showed better performance in terms of sales and results. Overall, the quarter revenue declined by 24% whereas the profit before tax declined by 34% year on year.

On the other hand, there is a positive trend and better performance at operational level in terms of clinker production, heat consumption, alternative fuels consumption, among others. Efficiency and quality improvement played a vital role in this quarter's performance, and we remain loyal to our top priority, which is customer centricity.

**Prospects**

In spite of cement demand slowing down in the first quarter, we are optimistic about market recovery in the coming months.

**Appreciation**

The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPC PLC will continue to deliver value for the shareholders and community.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
Chairman of the Board

### STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE PERIOD ENDED 31 MARCH 2024

| TZS '000 | 2024 | 2023 |
|---|---|---|
| Revenue from contracts with customers | 102,652,662 | 135,892,258 |
| Cost of sales | (76,425,963) | (96,140,826) |
| **Gross profit** | **26,226,699** | **39,751,432** |
| | | |
| Other operating income | 151,228 | 242,248 |
| Selling and marketing expenses | (823,567) | (718,016) |
| Administrative expenses | (5,291,684) | (5,621,153) |
| Other operating expenses | (308,742) | (409,355) |
| **Operating profit** | **19,953,934** | **33,245,156** |
| | | |
| Finance income | 706,866 | 1,082,485 |
| Finance costs | (175,005) | (161,611) |
| Net gain on foreign currency translation | 2,608,989 | 922,646 |
| **Profit before tax** | **23,094,784** | **35,088,676** |
| | | |
| Income tax expense | (7,090,142) | (10,757,897 |
| **Profit for the year** | **16,004,642** | **24,330,779** |

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 MARCH 2024

| TZS '000 | 2024 | 2023 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| **Non-current assets** | | |
| Property, plant and equipment | 137,809,294 | 139,954,546 |
| Intangible assets | 850,685 | 797,217 |
| Leasehold land | 946,124 | 973,970 |
| Right of Use assets | 171,835 | 3,501,560 |
| Other financial assets | 214,000 | 564,000 |
| | **139,991,938** | **145,791,293** |
| **Current assets** | | |
| Inventories | 82,956,165 | 88,086,153 |
| Trade receivables | 55,729,598 | 65,327,973 |
| Other short-term operating receivables | 20,439,804 | 23,047,980 |
| Other financial assets | 540,000 | 600,000 |
| Current income tax receivable | 4,914,367 | - |
| Cash and cash equivalent | 150,165,921 | 111,181,738 |
| | **314,745,720** | **288,243,844** |
| | | |
| **TOTAL ASSETS** | **454,737,793** | **434,035,137** |
| | | |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | |
| **Equity** | | |
| Authorised, issued and fully paid-up share capital | 3,598,462 | 3,598,462 |
| Retained earnings | 340,963,931 | 320,471,391 |
| **TOTAL EQUITY** | **344,562,393** | **324,069,853** |
| | | |
| **Non-current liabilities** | | |
| Lease liabilities | 194,450 | 194,450 |
| Employment benefit liabilities | 6,033,334 | 5,502,204 |
| Provision for quarry site restoration | 4,821,046 | 4,485,490 |
| Deferred income tax liability | 9,613,819 | 9,322,437 |
| | **20,662,649** | **19,504,581** |
| **Current liabilities** | | |
| Lease liabilities | - | 3,614,921 |
| Current income tax payable | - | 9,289 |
| Trade and other payables | 76,207,649 | 70,942,631 |
| Provisions | 10,583,245 | 13,049,775 |
| Dividend payable | 2,721,857 | 2,844,085 |
| | **89,512,751** | **90,460,703** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **454,737,793** | **434,035,137** |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Familia zirejee katika msingi wa malezi bora kwa watoto

**KUNA** msemo kwamba familia bora huzaa jamii bora na jamii bora huzaa taifa bora na lenye ustawi. Hakuna ubishi kwamba kama familia itakuwa imara na jamii itakuwa imara na hatimaye taifa litakuwa na maendeleo, amani, umoja na mshikamano.

Kila ifikapo Mei 15, kila mwaka, hufanyika maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani. Ni siku ambayo watu duniani kote hujadili na kuchambua masuala yahusuyo familia na changamoto zinazozikabili ili kutafuta njia za kuzitatua.

Wakati juzi siku hii adhimu iliadhimishwa, wadau mbalimbali walitoa maoni yao kuhusu namna bora ya kuleta ustawi wa familia ikiwamo malezi bora. Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliwasihi wazazi na walezi kuwa na utaratibu wa kufanya vikao vya familia ambavyo vitawasaidia kuzungumza na watoto ili kubaini vitendo vya ukatili wa kijinsia wanavyofanyiwa na jamaa wa karibu.

Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) nacho kiliishauri serikali kutunga sera ya familia ili kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, udhalilishaji watu na vifo vitokanavyo na matukio hayo.

Dk. Gwajima, katika maadhimisho hayo juzi jijini Dodoma, alisema moja ya sababu zinazochangia kwa kiasi kikubwa ukatili wa kijinsia kwa watoto ni wazazi na walezi kutokuwa na muda wa kuzungumza na familia zao na kuweka muda mwingi kwenye utafutaji wa maisha.

Ni ukweli usiopingika kwamba harakati za kutafuta maisha zimechangia kwa kiasi kikubwa wazazi kutokuwa na muda na familia na matokeo yake watoto wanajilea au wafanyakazi wa ndani kuwa ndio walezi wakubwa.

Baba na mama wanaamka asubuhi kwenda kwenye shughuli zao za kila siku bila kujua watoto wameamkaje, wamekwendaje shuleni na wamerudije nyumbani. Wakati mwingine baba anaweza kukaa hata wiki nzima hajaonana na watoto na hata siku za mapumziko anakuwa na vikao vingi vya kijamii.

Aidha, kutokana na kutumia muda mwingi katika utafutaji, baadhi ya wazazi wamewapeleka watoto katika shule za bweni wakiwa na umri mdogo. Watoto watasoma shule za bweni kuanzia elimu ya msingi mpaka vyuo vikuu na matokeo yake wanakosa malezi ya wazazi.

Licha ya majukumu ya utafutaji, kumekuwa na migogoro mingi katika ndoa ambayo imesababisha familia nyingi kusambaratika, hivyo kuathiri malezi na makuzi ya watoto. Hatua hiyo imesababisha kuibuka kwa malezi ya upande mmoja, hivyo watoto kukosa upande mwingine wa malezi ya wazazi.

Jambo hili limewajengea baadhi ya watoto kuwa na tabia zisizofaa katika jamii ndiyo maana kumekuwa na makundi ya uhalifu kama vile 'komando yoso', 'kiboko msheli', 'panya road', 'wadudu' na 'tukale wapi' ambayo yamesababisha uharibifu wa mali na hata kugharimu maisha ya watu. Sababu kubwa ni kwamba vijana hao wametengenezwa kuwa katika tabia na mienendo hiyo kutokana na yale waliyojifunza kutoka kwa wazazi na walezi wao.


Kama alivyosisitiza Waziri Gwajima, ni wakati mwafaka sasa kwa familia kurejea katika wajibu wao katika suala zima la malezi ya watoto ili kuokoa kizazi cha sasa na kijacho. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kuwarejesha Watoto katika misingi iwapasavyo na wataishi katika njia nzuri kwenye maisha yao.

Katika kufanya hivyo, familia zifanye vikao na kuzungumza na watoto wao ili kuwajengea uwezo wa kujiamini na kujua changamoto zinazowakabili katika maendeleo yao ya kitaaluma na maisha kwa ujumla.

Vikao hivyo pia vitawaandalia maisha ya baadaye hasa katika ujenzi wa familia zao kwa sababu watafikia umri wa kuwa waume au wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kwa kugusa kipaumbele hiki, vifo vya uzazi vitapungua

**VIPAUMBELE** vya Wizara ya Afya katika makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya mwaka 2024/25, ni kugharamia huduma ya afya ya uzazi, mama na mtoto, ili kuendelea kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga.

Waziri Ummy Mwalimu, ametaja vipaumbele kumi kikiwamo hicho wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake, bungeni jijini Dodoma wiki hii.

Ummy amewasilisha makadirio ya mapato na matumizi, wakati vifo vinavyotokana na uzazi na vifo vya watoto wachanga vikiwa ni miongoni mwa changamoto iliyokuwa imekumba nchi kwa miaka ya nyuma, ingawa kadri miaka inavyokwenda vinapungua.

Kupungua vifo hivyo, kunatajwa katika Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania ya Mwaka 2022, iliyozinduliwa mwishoni mwa mwaka jana, ikionyesha kuwa vifo vinavyotokana na uzazi vimepungua.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa vifo hivyo vimepungua kutoka 530 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/2016, hadi kufikia 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022.

Kupungua kwa vifo hivyo, kulielezwa kuwa ni juhudi zinazofanywa na wizara hiyo ya kusimamia huduma ya afya kwa weledi na umakini kuepusha vifo vinavyoepukika wakati wa hatua za kujifungua.

Wakati vifo hivyo vikiendelea kupungua, wizara nayo imetaja vipaumbele kumi katika bajeti ya mwaka 2024/25, kikiwamo hicho cha kuimarisha mifumo ya ugharimiaji wa huduma za afya lengo likiwa ni kuendelea kupunguza idadi ya vifo vya aina hiyo.

Kwa kuwa wizara inaeleza kuwa itagharimia huduma ya afya ya uzazi, mama na mtoto ili kuendelea kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga, ni wazi vitaendelea kupungua au kuisha.

Inaumiza kuona, baadhi ya watu wanapoteza wapendwa wao wakati wa kujifungua, lakini kwa kuwa dhamira ya serikali ni kuokoa maisha ya mjamzito na mtoto wake, ninaamini vifo vinavyotokea katika mazingira hayo vinaweza kuendelea kupungua.

Kuna sababu kadhaa, ambazo huwa zinatajwa kuchangia vifo hivyo, ikiwamo uzembe wa watoa huduma, uhaba wa wakunga na manesi, lakini pia baadhi ya wajawazito hutajwa kuchangia vifo vyao.

Wizara imeamua kugusa huduma ya afya ya uzazi, mama na mtoto katika vipaumbele vyake, ili kuendelea kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga.

Aidha, vipaumbele vingine ni kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa na upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa.

Eneo lingine, wizara hiyo imepanga kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalamu katika sekta ya afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi na huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi.

Vilevile, inatarajia kuendeleza na kusimamia afua za tiba asili na tiba mbadala na kuimarisha upatikanaji wa huduma za magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko.

Pamoja na hivyo, Wizara ya Afya, inakusudia kuimarisha huduma ya afya ya akili, huduma za wazee na watu wenye ulemavu na kusimamia utafiti na matokeo ya utafiti mbalimbali wa afya.

Vipaumbele vyote ni muhimu, lakini kuepusha vifo, ninadhani ni muhimu zaidi, kwani kujifungua ni jambo endelevu, hivyo, kuzuia vifo vitokanavyo na ujauzito na watoto wanaozaliwa ni kuendeleza kizazi.

Bajeti ya Wizara ya Afya imekuwa ikiongezeka kila mwaka wa bajeti, kitendo kinachoonyesha wazi kuwa wizara hiyo imedhamiria kuimarisha afya na kuokoa maisha ya Watanzania.

Kwa mfano, bajeti ya mwaka 2022/23, ilikuwa Sh. trilioni 1.109, mwaka uliofuata wa 2023/24, bejeti hiyo ilipanda hadi kufikia Sh. trilioni 1.235, sasa katika bajeti ya mwaka 2024/25 imefikia Sh. trilioni 1. 31.

Binafsi ninaamini kwamba hatua ya kuongezeka kwa bajeti hiyo, lengo lake ni kuendelea kuimarisha huduma za afya nchini, hasa katika maeneo ambayo bado yana changamoto yakiwamo yaliyopewa kipaumbele.

## HABARI KITAIFA

# Tembo kunufaisha wakazi wa vijijini

**Na Jenifer Gilla**

TEMBO wanaovamia makazi na mashamba sasa kuwa fursa kiuchumi kwa wakazi wa vijijini, serikali imesema.

Katika kuhakikisha wanyamapori waharibifu kama tembo hawaonekani tatizo bali fursa kwenye vijiji vyenye shoroba, serikali imeweka mkakati wa kutambua shoroba hizo ili kuwanufaisha wenyeji kiutalii na uchumi.

Hatua hiyo inatajwa inafanya wananchi washiriki katika kutunza wanyamapori hao badala ya kuwadhuru.

Mikakati hiyo imekuja kipindi ambacho matukio ya wanyamapori kuingia kwenye makazi ya watu na kufanya uharibifu yanazidi kuongezeka katika vijiji vyenye shoroba na kuchochea migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Idara ya Wanyamapori Wizara ya Maliasili na Utalii, Fortunata Msofe, mikakati hiyo inahusisha kuzitambua shoroba katika vijiji na kuzipa hati ili zitumike katika shughuli za uhifadhi, ikiwamo utalii wa kuwinda na picha na kuwanufaisha wakazi wa maeneo hayo.

Alibainisha hayo mwanzoni mwa wiki wakati wa mdahalo na waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET).

Alisema tayari wametambua shoroba 61 za wanyamapori nchini. Kati yake, wamesharasmisha shoroba 20 muhimu ambazo zina mwingiliano mkubwa kati ya binadamu na wanyamapori.

Alisema wameshatoa pia hati za matumizi ya rasilimali katika hifadhi za jamii za wanyamapori 22 zilizofikia vigezo na nyingine 16 zinakamilisha mchakato ili zikabidhiwe hati hizo na zinufaike na kuwapo rasilimali hiyo katika maeneo yao.

Alitaja mkakati mwingine ni kuhakikisha maeneo yenye shoroba yanaweza kufanya mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kupunguza mwingiliano kati ya binadamu na wanyamapori.

Alisema kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), wanatoa elimu kwa maeneo yenye shoroba juu ya umuhimu wa kuwatunza wanyamapori wanaopita katika maeneo yao na kuwaelekeza shughuli za kiuchumi za kufanya ili wasiingie tamaa ya kuwinda rasilimali hiyo.

Katika kuhakikisha mikakati hiyo inafanyika ipasavyo, ofisa huyo alisema mwaka 2022 waliandaa Mpango wa Mkakati wa Kuziongoa Shoroba za Wanyamapori wa Miaka Mitano wenye lengo la kuzitambua rasmi, ili kuruhusu wanyama wapite katika vijiji husika na wananchi wanufaike.

Pia iliundwa timu ya kitaifa inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu yenye wawakilishi kutoka wizara za kisekta ili kuhakikisha malengo ya wizara hizo yanazingatia uongoaji wa shoroba hizo.


"Wizara ya Ardhi inatusaidia kuhakikisha vijiji vyetu vinapimwa, kupitia upimaji huo wanatambua maeneo ya shoroba za wanyamapori na kufanya tathmini ya mapori tengefu ili kuyapandisha hadhi kuwa mapori ya akiba," alisema.

Ofisa Wanyamapori Mkuu na Mratibu wa Maliasili, Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi TAMISEMI, Hawa Mwechaga, alisema majukumu yao ni kuhakikisha wanavijiji wananufaika na rasilimali zao ili wazitunze kwa ajili ya kuhifadhi mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kuwa hivi sasa serikali inawekeza kwenye biashara ya hewa ukaa ambayo mapato yanayopatikana yanawanufaisha wakazi wa maeneo hayo na serikali inapata kodi .

"Kwa mfano, katika Halmashauri ya Tanganyika, vijiji vinane vinakwenda kupokea Sh. bilioni 14 kupitia biashara ya hewa ukaa, watu 250 wamepata ajira, wananchi wana bima za afya na kumejengwa hospitali kupitia biashara hiyo," alisema.

Ni mkakati inaohusisha pia kuwajengewa uwezo wananchi juu ya umuhimu wa kutunza miti ili wanyama wasihame na wao waendelee kunufaika kupitia utalii.



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KATAVI
*(AT MPANDA)*

CRIMINAL CASE NO 6926 OF 2024
THE REPUBLIC

VERSUS

AGREY SAMWEL MAUMBI

To:

Agrey Samwel Maumbi
Sumbawanga
**Rukwa Region**

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 23rd day of May 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of APRIL 2024

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE COURT
KATAVI

This summons has been issued on the Application of the Prosecution


Duplicate Served Upon Me:

Name……………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………………



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF SHINYANGA
*(AT SHINYANGA)*

CRIMINAL CASE NO. ……11588……OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

MOSHA SAMANGA……………………………………ACCUSED PERSON

To:

Mosha Samanga
Iponya Ward, Kagongwa Area,
Kahama District
**Shinyanga Region – 0754 294 143**

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT, CAP. 235 OF THE LAWS AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 29th day of ……MAY…… 2024……at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this ……2nd……day of ……MAY…… 2024……


RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name……………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship
Date……………………………………



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE DISTRICT MAGISTRATE'S COURT OF ILEMELA
*(AT ILEMELA)*

CRIMINAL CASE NO. 11364 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

MWITA STEVEN WAITARA ……………………ACCUSED PERSON

To:
Mwita Steven Waitara
Plot No. 256, Block A,
Nyamongolo Area, Ilemela District,
Mwanza City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 28TH day of MAY 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 30TH day of APRIL 2024

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
ILEMELA DISTRICT COURT.


This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name……………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………………



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF SHINYANGA
*(AT SHINYANGA)*

CRIMINAL CASE NO. ..11590.. OF 2024………

THE REPUBLIC

VERSUS

MASURE JINESA KIMBULU……………………………ACCUSED PERSON

To:
Masure Jinesa Kimbulu
Ndunguru Village
Kahama District

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 29th day of ……MAY…… 2024……… at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this ……2nd…… day of ……MAY…… 2024………

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
P.O. BOX 29 SHINYANGA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name……………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………………

# Nazi fursa mpya ajira kwa vijana

**Na Maulid Mmbaga**

KITUO cha Utafiti wa Kilimo (TARI) Mikocheni kimekuja na mikakati ya kufufua na kuinua zao la nazi kwa kuendesha utafiti, kutenga ardhi na fedha kwa ajili ya vikundi vya vijana watakaokuwa na utayari wa kujihusisha na kilimo cha zao hilo nchini.

Meneja wa TARI Mikocheni, Dk. Fred Tairo, aliwaambia waandishi wa habari juzi Dar es Salaam kuwa serikali inataka kutoa ajira kwa vijana ndio maana imetenga fedha kwa ajili ya kuhamasisha wajiunge kwenye vikundi, wasajiliwe ndani ya wilaya zao na kuungana na TARI kupatiwa mafunzo ya kuendesha vitalu kibiashara.

Alisema baada ya vijana hao kupata mafunzo, watakabidhiwa eneo katika vituo vyao vilivyoko nchi nzima, mbegu na msaada wa kifedha kwa ajili ya huduma za kilimo mpaka watakapofikia hatua za kuvuna na kuuza, na kwamba fedha itakayopatikana watarudisha kiasi na nyingine wataitumia kujiendeleza.

Alisema kuwa ili kuongeza kasi ya usambazaji mbegu bora kwa wakulima, wanashirikiana na wakurungezi wa halmashauri na kuweka makubaliano na wilaya kutoa eneo kwa ajili ya kuanzisha vitalu ambavyo vitatunza mbegu zitakazogawiwa kwa wakulima.

Alisema mkakati wao ni kuhakikisha kilimo cha nazi kinafufuka na kufikia malengo ambayo serikali inatarajia, akieleza kuwa uzalishaji wa zao hilo nchini umeshuka kwa kiwango kikubwa kulinganisha na miaka iliyopita licha ya uhitaji wa bidhaa zinazotokana na zao hilo kuwa mkubwa.

Ofisa Kilimo Msaidizi Mkuu TARI Mikocheni, Vaileth Kiwia, alisema zao la nazi ni muhimu kwa Tanzania kwa kuwa linahitajika katika chakula na kutengeneza thamani mbalimbali ambazo zina soko kubwa linalotoa fursa za ajira ndani na nje ya nchi.

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF SHINYANGA

*(AT SHINYANGA)*

CRIMINAL CASE NO. 11589 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

SOUD NASSOR ...............ACCUSED PERSON

To:
Soud Nassor
Kabanga Area, Luhumbo Ward
Shinyanga Rural District
Shinyanga Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 29th day of MAY 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of MAY 2024

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE P.O. BOX 29 - SHINYANGA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name
Signature
Qualification/Relationship
Date

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE DISTRICT MAGISTRATE'S COURT OF NYAMAGANA

*(AT NYAMAGANA)*

CRIMINAL CASE NO. 5046 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

ANNA LOUIS MALALE...............ACCUSED PERSON

To:
Anna Louis Malale
Plot No. 81, Block J, Nyegezi Area
Nyamagana District, Mwanza

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 27th day of MAY 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of APRIL 2024

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE MWANZA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name
Signature
Qualification/Relationship
Date

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA

*(AT MWANZA)*

CRIMINAL CASE NO. 5059 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

JOSEPH GETMAN MWANDWANGA...............ACCUSED PERSON

To:
Joseph Getman Mwandwanga
Mehama Street, Ilemela
Mwanza City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 28th day of MAY 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 30th day of APRIL 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE ILEMELA DISTRICT COURT.

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name
Signature
Qualification/Relationship
Date

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE DISTRICT MAGISTRATE'S COURT OF ILEMELA

*(AT ILEMELA)*

CRIMINAL CASE NO. 5058 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

ROBERT PIUS MASHUGA...............ACCUSED PERSON

To:
Robert Pius Mashuga
Plot No. 1723, Block B, Busimgwa Area
Ilemela, Mwanza Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 28th day of MAY 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 30th day of APRIL 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE ILEMELA DISTRICT COURT.

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name
Signature
Qualification/Relationship
Date

---

## NEEC yazindua 'Imarisha Uchumi na Mama Samia'

**Na Frank Monyo**

BARAZA la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limezindua Programu ya 'Imarisha Uchumi na Mama Samia' katika Mkoa wa Morogoro, lengo likiwa kutambua vikundi vya kinamama na makundi mengine ili kunufaika na shughuli zao.

Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng`i Issa aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi huo na kuongeza kuwa pia programu hiyo inalenga kukwamua kinamama kupitia vikundi vyao na makundi mengine ya Watanzania.

Alifafanua kuwa baraza lake linawaratibu katika kila mikoa na wanatumika katika kufanyakazi ya kusaidia makundi hayo kuingia katika kanzidata zao ili hatimaye waweze kunufaika na uwezeshaji utakaotolewa na programu hiyo.

Programu hiyo imekuja kuboresha shughuli zao za kilimo na zote za kijasiriamali wanazofanya ili kuwawezesha Watanzania kuwa na maisha bora.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema uzinduzi wa programu hiyo ni hatua muhimu kwa mkoa wake na hiyo ni moja ya hatua ya serikali katika kufanya Watanzania kufanya shughuli za ujasiriamali kwa tija.

Alifafanua kuwa mkoa wao utatekeleza programu hiyo kwa vitendo ambavyo itasaidia kuwawezesha Watanzania kufanya shughuli za uzalishaji.



# TAMISEMI yakemea tabia watumishi kufua kwa mikono

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imepiga marufuku wafanyakazi katika hospitali na vituo vya afya nchini kufua nguo kwa mikono, badala yake imewataka watumie mashine ili kuwaepusha kupata maambukizi ya magonjwa.

Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Dk. Rashid Mfaume, alitoa katazo hilo wakati akizungumza na waganga wakuu wa wilaya na wakuu wa idara za halmashauri za Mkoa wa Manyara.

Alitoa agizo hilo baada ya kutembelea Hospitali ya Mji wa Babati ya Mrara na kukuta uchafu katika maeneo ya Kituo cha Afya Daudi kilichopo katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu.

Alisema TAMISEMI haitakubali kuona wafanyakazi wanafua nguo kwenye vituo vya afya na hospitali kutumia mikono kwa kuwa wanaweza kupata magonjwa ya mlipuko.

Hata hivyo, alisema wanapaswa kujitathimini kwenye vituo vyao na wafuatilie kwenye hospitali za binafsi na vituo vya afya ili wasiruhusu kutumia mikono wakati wa kufua.

Pia, alisema hajaridhika na timu ya usimamizi wa huduma za afya ya Hospitali ya Mrara kwa kuwa kuna uchafu.

Vile vile, aliwaonya wafanyakazi wenye kauli chafu na wanaoibua maneno ya uchonganishi dhidi ya waganga wakuu wa wilaya.

Ofisa Afya na Mazingira, Suzana Nchalla, alisema maofisa afya wa wilaya na kata wanasahau kukagua maeneo ya nyumba za kulala wageni.

Hivyo, aliwaagiza maofisa afya wa wilaya na kata kufanya msako nyumba za kulala wageni na kuwapiga faini ambao hawafanyi usafi.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Dk. Damas Kayera, alisema vifo vitokanavyo na uzazi kwa mwaka jana vilikuwa 68 lakini wanaendelea na jitihada za kuvidhibiti.

Dk. Kayera alisema magonjwa yanayosumbua mkoa hapo ni ya mfumo wa hewa na kuhara.

**TAMISEMI haitakubali kuona wafanyakazi wanafua nguo kwenye vituo vya afya na hospitali kutumia mikono kwa kuwa wanaweza kupata magonjwa ya mlipuko.**

# Afungwa jela miezi sita kwa kufunga ofisi ya kijiji

**Na Allan ISACK,** SIMANJIRO

MKAZI wa Kijiji cha Okutu wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Melkzedek Moikani (33), amehukumiwa kwenda jela miezi sita kwa kufanya fujo, kufunga ofisi ya kijiji hicho.

Melkzedek ambaye ni mshtakiwa wa pili katika shauri hilo na wenzake watatu walishtakiwa kwenye Mahakama ya Wilaya ya Simanjiro kwa kutenda kosa hilo Januari 28 mwaka huu majira ya saa tisa alasiri.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Okutu, Neema Gelpeter, alikuwa mlalamikaji kwenye kesi hiyo.

Hakimu wa mahakama hiyo, Evarest Mushi, alimuhukumu mshtakiwa wa pili Melkzedek kifungo cha miezi sita bila faini na kuwaachia washtakiwa wengine watatu baada ya kudhibitika kuwa hawana hatia.

Washtakiwa wengine kwenye kesi hiyo Said Mdachi (65), Tumburu Jembe (40) na Seuri Moikani (43).

Hakimu Mushi alisema washtakiwa hao walitenda kosa la kufanya fujo kwa kufunga ofisi ya kijiji kinyume na Kifungu cha Sheria Namba 89 (12) ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

Alisema washtakiwa hao walifanya fujo kwa kufunga ofisi ya Mwenyekiti wa Kijiji kwa kutumia kufuli aina ya Solex yenye rangi ya fedha.

Pia, alisema washtakiwa hao walifunga Ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Okutu kwa kutumia kufuli yenye rangi ya shaba, hivyo kusababisha hofu kwa viongozi hao na kuwakwamisha kufanya shughuli za kijiji.

Hata hivyo, mshtakiwa wa kwanza, pili, tatu na nne upande wa mashtaka ulishindwa kudhibitisha mashtaka dhidi yao, hivyo waliachiwa huru.



Mwenyekiti wa kikundi cha Nyanza Group cha mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Malimi Kija (katikati) akizungumza wakati wakikabidhi unga, mchele, mafuta, sabuni na taulo za kike, kwa ajili ya watoto yatima na waliokuwa wakiishi kwenye mazingira magumu wa kituo cha Light In Africa juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanahisa CRDB kupata gawio 50/- kila hisa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANAHISA wa Benki ya CRDB wanatarajiwa kupata gawio la Sh. 50 kwa kila hisa kwa mwaka 2023 baada ya benki hiyo kurekodi ongezeko la faida.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya CRDB, Dk. Ally Laay, benki hiyo ilipata faida baada ya kodi Sh. bilioni 423 mwaka 2023 kulinganisha na Sh. bilioni 351 mwaka 2022.

Kutokana na faida hiyo, Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wa benki uliopangwa kufanyika Jumamosi jijini hapa, pamoja na mambo mengine, unatarajiwa kupitisha pendekeo hilo la ongezeko la gawio kwa hisa linalotokana na benki kuendelea kupata matokeo mazuri sokoni.

Mkutano huo umepangwa kufanyika kesho kuanzia saa 2:00 asubuhi katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

Ajenda mbalimbali zitajadiliwa katika mkutano huo, ikiwa ni pamoja na uchaguzi wa wajumbe huru wa bodi, kuteua wakaguzi wa hesabu, kujadili na kupokea Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi, Taarifa ya Hesabu Zilizokaguliwa na gawio kwa mwaka 2023.

Ni mkutano unaofanyika kufuatana na Sheria ya Kampuni Na. 212 ya Mwaka 2002, ambapo kila mwaka Benki ya CRDB imekuwa inaandaa mkutano huo unaowapa wanahisa fursa ya kujadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupitisha au kuidhinisha uamuzi mbalimbali wenye maslahi kwa benki.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Laay, alisema jana kuwa mkutano huo utafanyika kwa njia mseto ili kutoa fursa kwa wanahisa wengi zaidi kushiriki kwa njia ya kidijiti.

Dk. Laay alisema kupitia mtandaoni, wanahisa watawezа kujiunga kuanzia saa 2:00 asubuhi kupitia tovuti ya benki hiyo au mfumo wa benki hiyo waliopakua katika simu au kompyuta zao.

"Tumeweka mwongozo wa jinsi ya kushiriki mkutano mkuu kwa njia ya mtandao kupitia tovuti yetu, mitandao yetu ya kijamii, pia maelekezo yametumwa kwa ujumbe mfupi kwa wanahisa," alisema Dk. Laay huku akiwahakikishia kuwa benki hiyo vizuri katika kuhakikisha wanashiriki bila changamoto yoyote.

Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB utatanguliwa na semina maalum kwa wanahisa na umma itakayofanyika leo kuanzia saa tatu asubuhi huko AICC.

Dk. Laay alisema semina hiyo ambayo pia itaambatana na maonesho ya wanufaika wa programu ya IMBEJU itafunguliwa na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema katika mkutano mkuu wa 29 wanahisa wa benki hiyo watapata nafasi ya kujadili juu ya mwaka mmoja wa utekelezaji mkakati mpya wa biashara wa muda wa kati wa miaka mitano wa 2023 - 2027.

Nsekela alitumia fursa hiyo pia kuhamasisha wanahisa wa Benki ya CRDB kujitokeza kwa wingi kwa kuwa ushiriki wao utawezesha Bodi na Menejiment kupata maoni yao ya namna bora ya kuboresha utendaji wetu.



# Madiwani waagiza POS zipelekwe mashineni

Na Elizabeth Seleman, SENGEREMA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Sengerema mkoani Mwanza wameitaka Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kuweka mashine za ukusanyaji mapato katika kila mashine ya kukoboa mpunga.

Wamesema kwa kufanya hivyo itasaidia kukusanya ushuru wa mazao yanayoingia na kutoka mashineni.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Baraza hilo, Yanga Makanga, wakati wa kikao cha robo ya tatu ya mwaka 2023/24 na kusema kuwa hatua hiyo itasaidia pia kuongeza mapato katika halmashauri.

Alisema halmashauri inapoteza mapato kwa sababu mashine hizo hazina POS ya kukusanya mapato ya mazao na kusababisha hasara.

Aidha, alisema wanatakiwa kuwa na kikomo cha muda wa kuingiza mazao usiku kwenye mashine, ili yawe yanaingia mapema na kukatiwa ushuru na siyo muda wa usiku ambapo wakusanya ushuru wanakuwa wameondoka.

Yanga aliwataka wanaotoa mazao shambani kuandikiwa kibali na balozi wa eneo husika, ili waweze kutambulika kuwa ni wakulima au wafanyabiashara akisema baadhi ya wafanya biashara hawalipi ushuru kwa kisingizio kuwa ni wakulima.

Diwani wa Kata ya Sima, Makoye Sengerema ambaye pia ni Mwenyekiti Msaidizi wa Halmashauri hiyo aliwaomba madiwani kwenda kusimamia miradi ya maendeleo pamoja na kuitisha vikao, kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kuacha kuuza chakula kwa bei ya chini.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Umma Kanda ya Ziwa, Godson Kweka akizungumza baada ya kumwapisha Diwani wa Kata ya Buzilasoga, Edina Bandihai aliwataka watumishi wa serikali kufuata maadili ya kazi pindi wanapotekeleza majukumu yao.

Alisema baadhi ya watumishi wamejisahau na kupoteza maadili ya kazi ikiwa ni pamoja na matumizi mabovu ya lugha mambo alilolitaja kuwa ni kinyume na maadili na taratibu za utumishi wa umma.



Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa habari Mkoa wa Shinyanga, Greyson Kakuru akisoma Risala kwenye Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa vyombo vya habari mkoani Shinyanga juzi, ambayo kitaifa yalifanyika Mei 3 mwaka huu Jijini Dodoma, na kumuomba Mkuu wa Mkoa huo Anamringi Macha kutoa Maagizo kwa Viongozi wa Serikali wasibinye uhuru wa habari na kutoficha taarifa kwa maslahi mapana ya Wananchi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Walia wenzao kutumikishwa mashambani

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

WANAFUNZI wa Kata ya Lyabukande wilayani Shinyanga, wameiomba serikali kuingilia kati tabia za baadhi ya wazazi kuwashawishi watoto wao kujiunga na vikundi vya vijana vinavyotumika katika kilimo kama vibarua ili kujipatia kipato.

Wamesema hali hiyo inasababisha uwapo wa utoro shuleni kwa baadhi ya wanafunzi.

Ombi hilo limetolewa juzi na Mwenyekiti wa Baraza la Watoto Shule ya Msingi Mwamakala, Balele Mathias, wakati wakijadili viashiara vinavyosababisha ukatili kwa watoto na hata kuzima ndoto zao, katika kikao kilichoandaliwa na shirika la WEADO.

Alisema vikundi hivyo vimekuwa sehemu ya ukatili kutokana na kuwatumikisha hadi wakati wa masomo, hali inayosababisha ongezeko la utoro na wakati mwingine kuzima ndoto za wanafunzi hao.

"Watoto wanalazimishwa kujiunga na vikundi hivyo ili wapate pesa ya kukidhi mahitaji ya shule na wanafunzi wengine hufikisha hata mwezi mzima hawafiki shuleni," alisema Balele.

Ofisa Elimu Kata ya Lyabukande, Juma Chiamba, alikiri kwamba kipindi cha msimu wa kilimo ni kweli wanafunzi wanakuwa watoro shuleni lakini siyo kwa kiasi kikubwa.

Alisema katika kipindi cha mavuno kumekuwepo na utoro wa rejareja unaosababishwa na utumikishwaji wanafunzi wakati wa masomo.

Alisema wanachokifanya ni kuendelea kutoa elimu kwa wazazi, kwamba siku za masomo wawaache watoto wao wasome na zile za mapunziko ndipo watumie muda huo kwenda kuvuna mazao shambani.

Baadhi ya wazazi wakizungumza katika mkutano huo walisema ni kweli baadhi yao wamekuwa wakiwazuia watoto wasiende shuleni ili wakalime vibarua kutokana na hali duni ya kimaisha.

Mkurugenzi wa Shirika la WEADO, Eliasenya Nnko, alisema wamefanya kikao hicho cha majadiliano na mabaraza ya watoto, walimu, walezi na viongozi wa kata ili kubaini viashiria ambavyo husababisha ukatili kwa watoto na kuvifanyia kazi.

Viashira vingine vya ukatili dhidi ya watoto vilivyotajwa kwenye kikao hicho vinatokea katika maeneo ya minadani, vibanda vya kuonyesha mpira, machungani, magurio, saluni za kunyoa nywele na vichakani wakati wa kukata kuni.

# Utendaji bora Bandari Dar es Salaam waikuna WFP

Na Faustine Feliciane

BANDARI ya Dar es salaam imepongezwa kwa utendaji kazi mzuri uliorahisisha huduma ya utoaji mizigo kwa taasisi, wafanyabiashara na mashirika ya kimataifa.

Pongezi hizo zimetolewa jana na Mkurugenzi Mkazi na Mwakilishi wa Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP), Sarah Gordon-Gibson, wakati akipokea msaada wa tani 25 za tende zilizoongezwa virutubisho kutoka kwa Serikali ya Saudi Arabia.

Alisema Bandari ya Dar es salaam imekuwa kituo kikubwa kwa WFP katika kusambaza huduma za kijamii kwa nchi mbalimbali Afrika.

"Bandari hii imekuwa ikifanya kazi nzuri sana, ni kituo kikuu kwetu katika kusambaza misaada kwa nchi mbalimbali Afrika, nawapongeza kwa kazi nzuri na ya haraka katika utoaji wa mizigo," alisema Sarah.

Akizungumzia msaada huo, Sarah, alisema Saudi Arabia wamekuwa mshirika mkubwa wa WFP katika kusaidia makambi mbalimbali ya wakimbizi.

Alisema msaada huo utaenda kutolewa kwa wakimbizi zaidi ya 200,000 wanaishi kwenye kambi za Nyarugusu na Nduta mkoani Kigoma.

Kwa upande wake, Balozi wa Saudi Arabia nchini Tanzania, Yahya Okeish, alisema msaada huo umetolewwa na Saudi Arabia kwa kuzingatia moyo wa kuwasaidia watu wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Alisema Saudi Arabia imekuwa ikitoa misaada ya kibinaadamu kwa nchi mbalimbali zenye uhitaji au makambi ya wakimbizi, kwamba wataendelea kufanya hivyo kulingana na mahitaji.

"Tutaendelea kushirikiana na WFP katika kuhakikisha tunawasaidia watu na kuwapa maisha mazuri, naipongeza pia Seriakli ya Tanzania kwa kushirikiana na WFP kuwahudumia wakimbizi," alisema Okeish.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA,) Dk.George Fasha alisema kuwa WFP imekuwa mshirika wa muda mrefu kati ya mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo yamekuwa yakitumia kikamilifu Bandari ya Dar es Salaam katika shughuli zake.

Alisema TPA itaendelea kutoa huduma bora kwa wateja washirika wake wakiwemo WFP.

Alisema: "Nawashukuru sana WFP kwa kuendelea kutuamini na kutupa ushirikiano, lakini pia niwapongeze na kuwashukuru Serikali ya Saudi Arabia kwa msaada huu unaoenda kuwasaidia ndugu zetu wakimbizi".

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

# HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25



**Mhe. Nape Moses Nnauye**
**Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.**



**Eng. Maryprisca Winfred Mahundi**
**Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.**



**Bw. Mohammed Khamis Abdulla**
**Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.**



**Bw. Nicholaus Merinyo Mkapa**
**Naibu Katibu Mkuu wa Wiraza ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.**





# HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25

**UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika***, Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) kwa Mwaka 2023/24, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/24. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka 2024/25.

**Shukrani na Pongezi**

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa kumi na tano wa Bunge la kumi na mbili.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake madhubuti kwa kipindi cha miaka mitatu tangu aingie madarakani na kuendelea kutuongoza vyema huku tukishuhudia maendeleo na uwekezaji mkubwa kwa Sekta zote hususan Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Wizara inatambua matarajio makubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais katika kufikishiwa huduma za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuongoza nchi yetu kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla.

5. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), kwa miongozo na uongozi wake makini katika kulisimamia Bunge na Serikali kwa ujumla.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, nikupongeze wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa weledi, busara, hekima na tija kusudiwa kwa kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa na ya wananchi yanajadiliwa kwa umakini. Pia, niendelee kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Muungano wa Mabunge Duniani (IPU) na Baraza la Uongozi la IPU. Hakika unastahili pongezi za kipekee kwa kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo tangu historia ya kuanzishwa kwa chombo hicho. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.) Naibu Spika, kwa kuendelea kukusaidia kuliongoza Bunge lako. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge lako Tukufu.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao kwangu na Wizara kwa ujumla katika kuhakikisha malengo ya sekta yanafikiwa. Pia ninaishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 68, kwa Mwaka 2024/25 na kuyapitisha kwa kauli moja. Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika Hotuba hii. Ninachoweza kuwaahidi kuwa maadam 'imani huzaa imani', mimi na wenzangu wizarani, tutakwenda kusimamia na kutekeleza maelekezo ya Kamati kikamilifu. Ninapenda kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu pamoja na wakati wa kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara. Ninapenda kuwahakikishia kuwa, Wizara ninayoingoza itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya Maendeleo ya Taifa na ya wananchi katika nyanja za kiuchumi na kijamii.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Ndugu Nicholaus Merinyo Mkapa kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ninayoiongoza.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee na umuhimu mkubwa naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtama kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kujiletea maendeleo kwenye Jimbo letu; bila kuisahau familia yangu kwa upendo, uvumilivu katika nyakati zote ambazo nimekua nikiendelea kutekeleza majukumu yangu.

**Salamu za Pole**

11. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii adhimu kutoa pole kwa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa *Dkt.* Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na kiongozi wetu Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika tutaendelea kumuenzi kwa umahiri wake na kwa mageuzi ya kisiasa aliyoyafanya, pamoja na kufungua nchi kiuchumi kwa kuruhusu uwekezaji wa sekta binafsi.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nitumie fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowasa aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hayati Lowassa ataendelea kukumbukwa kwa uthubutu wake, uwezo na ushawishi mkubwa katika kusimamia shughuli za Serikali.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa natoa pole kwako Mheshimiwa Spika na Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali kwa tiketi ya CCM na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Kwahani kwa tiketi ya CCM. Vilevile, naungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla, kutoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopatwa na majanga mbalimbali katika mwaka 2023/24, yakiwemo mafuriko na maporomoko ya mawe na matope katika maeneo ya Hanang Mkoani Manyara; Kibiti na Rufiji Mkoani Pwani pamoja na Malinyi, Ulanga, Ifakara, Mlimba Mkoani Morogoro na maeneo mengine nchini. Nipende kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na Watanzania wote walioondokewa na wapendwa wao. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**Wajibu wa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

14. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jukumu la kutunga na kusimamia Sera zinazohusiana na masuala ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuratibu na kusimamia vyombo vya Habari, Mawasiliano ya Posta na Simu; kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA; kuendeleza wataalam wa TEHAMA, kuanzisha na kusimamiana Postikodi, kuendeleza na kusimamia miundombinu ya Habari na Mawasiliano nchini ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Utekelezaji wa majukumu haya kutaiwezesha Tanzania kuimarika kushiriki uchumi wa kidijitali katika kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda ($4^{th}$, $5^{th}$ na $6^{th}$ Industrial Revolution) yanayochochewa na kuwezeshwa na matumizi ya TEHAMA ambayo yatasaidia kuwa na jamii inayopata taarifa sahihi kwa wakati ili wananchi waweze kushiriki katika kuleta maendeleo.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inasimamia Taasisi **tisa** ambazo zimegawanyika kwenye umahsusi wa Huduma, mashirika ya kibiashara, udhibiti, mfuko, baraza na taasisi wezeshi. Taasisi hizo ni: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Shirika la Mawasiliano Tanzania; Shirika la Posta Tanzania; Shirika la Utangazaji Tanzania; Kampuni ya Magazeti ya Serikali; Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; Tume ya TEHAMA; Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano. Hotuba hii itaelezea kwa ufupi masuala yanayotekelezwa na

Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**Hali ya Ukuaji wa Sekta ya Habari na Mawasiliano na Upatikanaji wa Mawasiliano Nchini**

16. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua ambapo takwimu zinaonesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka **milioni 62.3** Mwezi **Aprili, 2023** hadi kufikia laini **milioni 72.5** Mwezi **Aprili, 2024** sawa na ongezeko la **asilimia 16.4.** Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka **milioni 33.1** Mwezi **Aprili, 2023** hadi kufikia **milioni 36.8** Mwezi **Aprili, 2024** sawa na ongezeko la **asilimia 11.2.** Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka milioni **44.3** mwezi **Aprili, 2023** hadi kufikia Milioni **53.0** mwezi **Aprili, 2024** sawa na ongezeko la **asilimia 19.6.** Aidha, Watoa huduma wa Miundombinu ya Mawasiliano wamefikia **25** ukilinganisha na watoa huduma **23** Mwezi **Aprili, 2023** sawa na ongezeko la **asilimia 8.7**.

**Hatua iliyofikiwa ya Mapinduzi ya Uchumi wa Kidijitali**

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ina wajibu wa kusimamia Mapinduzi ya Kidijitali nchini. Mapinduzi ya Kidijitali yanaweka msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Katika Uchumi wa kidijitali, Sekta zote hufanya kazi kwa pamoja, kwa ushirikiano na muingiliano zikiwezeshwa na mazingira bora ya kidijitali. Ili kuharakisha Tanzania kuelekea katika uchumi wa kidijitali, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuanza kutumika kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Kanuni zake pamoja na uanzishwaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Hatua hii ni muhimu hasa ukizingatia kuwa mapinduzi ya kidijitali yanachochewa na matumizi ya taarifa (Data) ambayo imekua ni bidhaa adimu. Pia Serikali imepitisha Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali 2024-2034 utakaosaidia kuongeza matumizi ya kidijitali kwa huduma zinazotolewa na Serikali pamoja na Sekta binafsi. Mkakati huo una nguzo muhimu sita (6) zikiwemo uwezeshaji wa miundombinu ya Kidijitali, utawala wa Kidijitali na uwepo wa Mazingira wezeshi, kujenga uelewa na ukuzaji wa ujuzi wa kidijitali, uwepo wa utamaduni wa ubunifu wa kidijitali na teknolojia wezeshi, tamaduni ya ujumuishaji wa makundi maalum katika matumizi ya kidijitali na kuwezesha huduma za kifedha kwa kidijitali pamoja na maamuzi ya Serikali ya kuihamishia Mamlaka ya Serikali Mtandao kuwa moja ya Taasisi chini ya Wizara. Hatua hii itawezesha kuchochea ukuaji wa matumizi ya TEHAMA pamoja na ujenzi wa mifumo mbalimbali ya utoaji huduma kwa mujibu wa malengo na mwelekeo wa kisera. Katika hatua hii tunamshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Baraza la Mawaziri.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika safari hii ya mapinduzi ya kidijitali Wizara imeanza kufanya marejeo ya Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 pamoja na kuandaa 14 ya miongozo mbalimbali itakayotumika katika usimamizi wa Sekta ya TEHAMA ambayo itasaidia kuboresha utendaji kazi wa Taasisi kwa kutumia mifumo ya kidijitali, kuifanya Tanzania kuwa na viwango vinavyotambulika kimataifa katika TEHAMA, usimamizi wa misingi ya mageuzi ya kidijitali nchini, kujenga uelewa kwa wananchi wote kuhusu matumizi ya TEHAMA, ujumuishaji wa makundi ya anuai katika huduma za kidijitali, matumizi ya akili mnemba, Mkakati wa Usalama Mtandao *(Cyber Security Strategy)* pamoja na Mkakati wa Kufanya Tafiti na Bunifu za TEHAMA nchini.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Tanzania inapiga hatua zaidi katika uchumi wa Kidijitali, Wizara kwa kushirikiana na wadau muhimu inaendelea kuandaa mfumo jumuishi (*Samia's Technology Stack)* unaojumuisha mifumo mitatu (3) ambayo ni: ***Mfumo wa Jamii Namba*** ambao utatumika kufanya utambuzi wa kipekee wa kila mwananchi kuanzia anapozaliwa ambapo atakuwa na akaunti ya kidijitali itakayomwezesha kupata huduma zote za kijamii; ***Mfumo wa Jamii Malipo*** ambao utawezesha wananchi kutumia Jamii Namba kupokea fedha na kurahisisha kufanya malipo kidijitali. Mfumo huu pia utasaidia *Financial Inclusion* na kuongeza Wigo wa mapato ya Serikali; na ***Mfumo wa Jamii Data Shirikishi*** ambao unamwezesha mwananchi kumiliki taarifa zake katika kupokea huduma mbalimbali nchini. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao na Tume ya TEHAMA Nchini imeanza ujenzi wa Mfumo wa Ubadilishanaji taarifa uitwao Jamii Data Exchange Platform/ Tanzania Enterprise Service Bus.

**Hali ya Sekta ya Habari Nchini**

20. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha Sekta ya habari nchini ambapo vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo **65** mwaka 2023 na kufikia vituo **68 Aprili, 2024** sawa na ongezeko la asilimia **4.6** na *Cable Television* zimeongezeka kutoka **57 Aprili, 2023** na kufikia **60 Aprili, 2024** sawa na ongezeko la **asilimia 5.3**. Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo **215** mwaka 2023 hadi kufikia vituo **231 Aprili, 2024** sawa na ongezeko la **asilimia 7.4** na magazeti yameongezeka kutoka **321 Aprili, 2023** na kufikia **351 Aprili, 2024** sawa na ongezeko la **9.3**. Aidha, Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za utangazaji hasa maudhui mtandaoni ambayo pia yamechangia kuongeza ajira kwa vijana.

**Uhuru wa vyombo vya habari**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuhakikisha kuwa vyombo vya habari nchini vinakuwa huru kupokea na kutoa habari za matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii. Takwimu kutoka *World Press Freedom Index 2024* inayoratibiwa na Taasisi ya *Reporters without boarders (RWB)(RSF)* zimeonyesha kuwa Tanzania inaongoza Afrika Mashariki kwa kuheshimu uhuru wa habari, ambapo Kimataifa imeshika nafasi ya **97** Mwaka 2024 toka nafasi ya **142** Mwaka 2023 na kupelekea kupanda katika kuheshimu uhuru wa vyombo vya Habari. Mafanikio haya yametokana na Serikali kuchukua hatua muhimu ikiwemo Bunge lako Tukufu kufanya mabadiliko ya sheria ya huduma ya vyombo vya habari 2016 Mwaka 2023.

**Gharama za Mawasiliano ya Simu**

22. ***Mheshimiwa Spika***, Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa bei ya dakika ndani ya mtandao bila kifurushi (Shilingi/dakika) zimeendelea kushuka kutoka Shilingi **29.0** Juni, 2023 hadi kufika wastani wa Shilingi **26.00** Aprili, 2024, wakati bei ya dakika nje ya mtandao bila kifurushi imeshuka kutoka wastani wa Shilingi **31.0** Juni, 2023 hadi kufikia wastani wa Shilingi **28.00** Machi, 2024. Mwenendo wa gharama za rejareja za data bila kifurushi na kwenye kifurushi zimeendelea kupungua. Aidha, katika robo ya mwaka inayoishia Machi 2024, gharama za data ndani ya kifurushi zimeshuka na kufikia wastani wa Shilingi **2.17** kwa Mb Aprili, 2024 ikilinganishwa na Shilingi **2.25** kwa Mb Juni, 2023.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2023/24**

**Bajeti iliyoidhinishwa**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2023/24 Wizara iliidhinishiwa kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni 212.4.** Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 30.5** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni 18.5** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi bilioni 11.9** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, **Shilingi bilioni 181.9** ziliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo **Shilingi bilioni 146.8** ni fedha za ndani na **Shilingi bilion**i **35.2** ni fedha za nje.

**Fedha zilizopokelewa na Wizara**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 213.9** sawa na **asilimia 100.7** ya **Shilingi bilioni 212.4** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika Mwaka 2023/24. Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi **bilioni 16.3** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 7.0** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi bilioni 190.6** ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha za miradi ya maendeleo inajumuisha **Shilingi bilioni 102.1** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 88.5** ni fedha za nje.

**MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kufanya tathmini ya hali ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 na Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997 na kuandaa Rasimu ya Sera Mpya ya Taifa ya TEHAMA 2024;
ii. Kuandaa Rasimu ya Sera ya Kampuni changa za TEHAMA (Startups);
iii. Kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambayo ilizinduliwa tarehe 3 Aprili, 2024 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
iv. Kukamilisha kuhamisha shughuli zote za Ujenzi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Kuhifadhi Data (NIDC) kwenda Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL);
v. Kukamilisha ujenzi wa Kilomita **3,008** na Vituo **66** vya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
vi. Kukamilisha upanuzi wa Mkongo wa Taifa kutoka ukubwa wa 200Gbps kwenda 800Gbps kwenye mizunguko mikuu ya Mkongo wa Taifa na kuanza upanuzi wa Mkongo kutoka 800Gbps hadi 2000Gbps;
vii. Kuanza Ujenzi wa minara **758** katika Kata **731** na kuongeza uwezo wa minara **304** kutoka teknolojia ya 2G kwenda 2G/3G na 4G. Hadi Aprili, 2024 Minara **142** imekamilika kujengwa ambapo minara **124** tayari inatoa huduma. Aidha, minara **243** imeongezewa nguvu;
viii. Kukamilisha Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu

ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU) na kuzinduliwa rasmi tarehe 2 Septemba 2023 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jijini Arusha;

ix. Kukamilisha Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na kuzinduliwa rasmi tarehe 25 Aprili, 2024 na Dkt. Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jijini Dodoma;

x. Kukamilisha ujenzi wa miradi ya upanuzi wa usikivu wa redio za TBC katika maeneo saba ya Serengeti – Mara, Bariadi – Simiyu, Ileje – Songwe, Njombe, Kilwa – Lindi, Unguja na Pemba;

xi. Kukamilika, kuridhiwa na kuanza kutumika kwa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali 2024 – 2034 na Miongozo sita ya Usimamizi wa Sekta ya TEHAMA;

xii. Kukamilisha majadiliano kati ya Serikali na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano (consortium) kulikopekelea Serikali kulipwa Dola za Marekani **milioni 33**;

xiii. Kusainiwa kwa Mikataba ya mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na nchi za Uganda wenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 28.8**, Malawi wenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 5.5,** Burundi wenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 3.3** na Kampuni ya Airtel wenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 4.8**;

xiv. Kuunda Kamati ya Kitaifa ya usimamizi wa Setelaiti nchini kwa ajili ya kuratibu, kusimamia na kuendeleza shughuli za anga za juu nchini;

xv. Kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya TBC katika eneo la Vikonje Jijini Dodoma ambapo hadi Aprili, 2024 ujenzi umefikia asilimia **18**;

xvi. Kuanza ujenzi wa kiwanda kwa ajili ya kufunga mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji ambapo ujenzi umefikia asilimia **35**;

xvii. Kuongeza Ushiriki wa Tanzania kwenye masuala ya kikanda na kimataifa hasa kwa Mashirika hususani Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU), Shirika la Mawasiliano Afrika (ATU), Umoja wa Posta Afrika (PAPU) na Umoja wa Posta Duniani (UPU);

xviii. Kushinda tuzo ya ubora kwa Shirika la Posta Tanzania kutokana na kuandaa, kusimamia na kutekeleza miradi inayofadhiliwa na Umoja wa Posta Duniani;

xix. Kupata obiti mpya ya setelaiti ya $16^0$W kwa matumizi ya Satelaiti za Utangazaji na masafa mapya yatakayotumika katika kuboresha usalama wa mawasiliano ya angani na majini;

xx. Kuwezesha kupungua kwa gharama za uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano kwenye hifadhi za barabara ambapo ada ya awali imepungua kutoka Dola za Marekani **1000** hadi **200** kwa Kilomita na Ada ya mwaka imepungua kutoka Dola za Marekani **1000** hadi **100** kwa Kilomita;

xxi. Kuwezesha ujenzi na uzinduzi wa Kituo cha Mkongo wa Baharini wa 2Africa wenye uwezo wa kusukuma kiwango kikubwa cha intaneti kuanzia 17Tbps hadi 180Tbps;

xxii. Kuunganisha ofisi **50** za RUWASA kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

xxiii. Kuunganisha watumiaji **12,584** na huduma za faiba mlangoni;

xxiv. Kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Kituo cha kuhifadhi data Zanzibar;

xxv. Kuhakiki na kuboresha taarifa za Anwani za Makazi katika Halmashauri tano (5) ambazo ni Manispaa za Morogoro, Iringa, Singida, Kigoma Ujiji na Halmashauri ya Mji wa Masasi. Kupitia zoezi hili Anwani **2,308,231** (Tanzania Bara **1,937,111** na Zanzibar **371,120**) zimehakikiwa kati ya anwani **12,385,956** zilizokusanywa wakati wa operesheni. Vilevile, Anwani mpya **505,436** zimesajiliwa na kufanya idadi ya Anwani za Makazi zilisosajiliwa kuongezeka hadi **12,891,392** sawa na ongezeko la asilimia **4.1**;

xxvi. Kufanya maboresho ya mfumo wa Anwani za Makazi (NaPA) kuwezesha kutoa barua za utambulisho wa ukaazi kupitia Watendaji wa Kata na Shehia kidijitali. Moduli hii imezinduliwa Aprili 2024 kwa majaribio ambapo hadi sasa jumla ya barua **708** kutoka mitaa **152** zimeombwa na kutolewa;

xxvii. Kutoa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi **20** wa Serikali katika nchi za Ujerumani, Uingereza, Malaysia na Marekani. Aidha, Serikali imetangaza nafasi nyingine **480** za mafunzo ya muda mfupi kupitia mradi wa Tanzania ya kidijitali;

xxviii. Kudhibiti mawasiliano ya simu ambapo simu za ulaghai **767** zimebainika na hatua stahiki zimechukuliwa kwa mujibu wa Sheria;

xxix. Kuanza utekelezaji wa mradi wa Muundombinu wa Kitaifa wa Saini za Kielektroniki (NPKI);

xxx. Kukamilisha ujenzi wa maabara ya uidhinishaji wa vifaa vya mawasiliano ya kieletroniki (type approval laboratory), ambao unajumuisha maabara ya kupima mionzi inayotokana na simu za mkononi (specific absorption rate lab) na maabara ya kupima masafa ya kifaa (radio frequency lab)

xxxi. Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Miji Janja (Smart Cities) katika Majiji ya Dodoma, Arusha na Mbeya;

xxxii. Kupeleka huduma ya Wi-Fi uwanja wa Benjamin Mkapa, Viwanja vya sabasaba, Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (CoICT) Kijitonyama na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM);

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa majukumu mengine ya Sekta ya Habari, Mawasiliano na TEHAMA yameainishwa kwenye Ukurasa wa 19 hadi 42 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo katika mwaka 2023/24 Sekta binafsi zimeendelea kushirikiana na Wizara katika maeneo yafuatayo:

i. Hati ya mashirikiano kati ya Serikali na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano (Consourtium of Telco Operators) imefanyiwa maboresho na kusaini. Matokeo ya ushirikiano huu ni kujengwa kwa miundombinu ya Mkongo wa Mawasiliano katika Maeneo ambayo Mkongo wa Taifa haujafika na miundombinu hiyo iliyokamilika inatarajiwa kukabidhiwa kwa Serikali ili kujumuishwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

ii. Kampuni tano za Mawasiliano ya Simu zimechangia asilimia 60 ya gharama za ujenzi wa Minara 758 katika Kata 713 inayoendelea kujengwa sehemu mbalimbali nchini;

iii. Utoaji wa huduma ya intaneti kwenye maeneo ya wazi;

iv. Utoaji wa elimu kuhusu matumizi sahihi na salama ya mawasiliano;

v. Kuendelea kuanzisha televisheni na redio kwa lengo la kuwezesha kuhabarisha umma na kuharakisha bunifu za kidijitali; na

vi. Tumefanikiwa kuwezesha kusainiwa kwa hati ya ushirikiano kati ya Kampuni ya Airtel Tanzania na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kuunganisha Shule 3,000 na mtandao wa intaneti kwa kipindi cha miaka mitano.

**MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Mpango na Bajeti wa mwaka 2024/25 kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025; Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); na Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia Bunge tarehe 22 Aprili, 2021.

***Makadirio ya Mapato ya Wizara***

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/25, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 100,700,000,000** ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, usajili wa Magazeti, ada ya mwaka ya Magazeti, vitambulisho vya Waandishi wa Habari na machapisho ya picha, mabango na majarida.

***Malengo ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari***

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia Mapinduzi ya Kidijitali yanayowezeshwa na TEHAMA na pia kuimarisha mfumo wa kupashana habari kwa kusimamia uhuru wa vyombo vya habari nchini. Mapinduzi ya Kidijitali ndio yanayoweka Msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Ili kuwezesha mageuzi na mapinduzi haya kwenye Sekta zote za Uchumi na Kijamii, Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi imepanga kufanya mabadiliko na maboresho makubwa kwenye Sekta ili kuendana na mageuzi kwa kutunga na kuhuisha Sera, Sheria na Miongozo inayosimamia Sekta za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na Posta kote nchini, kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha Biashara Mtandao nchini, kuimairisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali, kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao, kuimarisha upatikanaji wa habari nchini, na kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni changa (Startups).

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2024/25 Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kukamilisha uhuishwaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003, Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 na kutunga Sera mpya ya Taifa ya TEHAMA ambayo itajumuisha masuala ya Kampuni changa za TEHAMA (Startups);

ii. Kuratibu utungwaji wa Sheria ya Anwani za Makazi;

iii. Kufanya mapitio ya Sheria ya usalama wa mtandao ya mwaka 2015 ili iendane na wakati wa sasa na pia iweze kujumuisha masuala ya kumlinda mtoto dhidi ya ukatili wa mtandaoni na masuala ya ugaidi

mtandaoni;

iv. Kukamilisha ujenzi wa minara ya mawasiliano ya Simu **616** ili kuweza kufikia minara **758** katika kata **713** pamoja na kuanza ujenzi wa minara mingine mipya **636** ili kuhakikisha maeneo yaliyobakia yanapata mawasiliano.

v. Kuiongezea nguvu minara **135** kutoka teknolojia ya 2G kwenda 2G/3G na/au 4G;

vi. Kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo **70** ya kimkakati mathalan maeneo ya hifadhi na mipakani;

vii. Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye Wilaya 40 nchini;

viii. Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika;

ix. Kuanza ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Data Dodoma na Zanzibar pamoja na kuanzisha Kituo kimoja cha Usalama wa Mawasiliano cha Taifa;

x. Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na vyombo vya ulinzi na usalama (Mahakama, TAKUKURU, Polisi, Magereza, JWTZ, Usalama) pamoja na taasisi 100 za Haki Jinai na Taasisi nyingine za Serikali;

xi. Kuendelea kuimarisha mifumo ya kusimamia na kupima ubora wa huduma za mawasiliano ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma na usimamiaji wa Sekta;

xii. Kuwezesha Mfumo wa Anwani za Makazi (NaPA) kuunganishwa na mifumo mingine ya kutolea huduma za kijamii;

xiii. Ununuzi wa magari mawili maalumu ya kurushia matangazo mbashara (OB Van) na magari 15 kwa ajili ya shughuli za utangazaji katika vituo vipya vya kurushia matangazo ikiwemo kuwezesha kutangaza shughuli za Uchaguzi Mkuu na wa Serikali za Mitaa;

xiv. Kuendelea na taratibu za kuanzisha Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari;

xv. Kuratibu uanzishaji wa Wakala wa Anga za Juu nchini (Tanzania Space Agency) na kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Anga za Juu (Outer Space Strategy);

xvi. Kutengeneza na kutumia mfumo wa kukusanya na kusambaza mizigo ("uberlike" pick and delivery system);

xvii. Kusimamia uundaji wa mfumo wa kidijitali utakaowezesha biashara Mtandao (e-Commerce);

xviii. Kutekeleza mradi wa kujenga kituo cha kikanda kitakachojumuisha maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao;

xix. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Muundombinu wa Kitaifa wa Saini za Kielektroniki (NPKI) ili kuhakikisha usalama wa miamala ya kielektroniki nchini;

xx. Kuendelea na uratibu wa uendelezaji wa Mifumo ya Kitaifa nchini;

xxi. Kujenga maabara za Akili Mnemba (AI) na matumizi ya Roboti nchini;

xxii. Kuendelea kuwezesha uanzishaji na ukuzaji wa vituo vya ubunifu vya TEHAMA katika Wilaya sita (6) kwa kuanzia (District ICT Startups Innovation hubs);

xxiii. Kuwaendeleza wataalam 30 wa TEHAMA kwenye programu za muda mrefu na wataalam 450 kwenye programu za muda mfupi;

xxiv. Kuanza ujenzi wa vyuo viwili (2) vya TEHAMA Nala - Dodoma na Buhigwe - Kigoma;

xxv. Kusajili wakusanyaji na wachakataji 500,000 wa taarifa binafsi;

xxvi. Kuendelea kuimarisha usikivu wa redio za TBC kwa kujenga mitambo ya redio yenye masafa ya FM kwenye Wilaya saba za Buhigwe, Malinyi, Lushoto, Buchosa, Mafia, Ikungi na Kaliua; na

xxvii. Kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha uchapaji na kufunga mitambo ya kisasa ya uchapaji.

***31. Mheshimiwa Spika,*** Mipango mingine ya Sekta ya Mawasiliano imefafanuliwa katika Ukurasa wa 43 hadi 57 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

**Mchango wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25**

***32. Mheshimiwa Spika,*** katika kuunga mkono juhudi za Serikali, kwa mwaka 2024/25 Sekta Binafsi imeridhia kutekeleza yafuatayo:

i. Kampuni za simu za Airtel Tanzania, Vodacom Tanzania, Honora Tanzania, Halotel na TTCL yamepanga kuendelea kushirikiana na Serikali kwenye ujenzi wa minara **616** ya mawasiliano ya simu kati ya minara **758** na kuendelea kuongeza uwezo kwenye minara **61** kati ya minara **304**. Aidha, kampuni hizi zimepanga kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa minara mipya **636** ya mawasiliano ya simu;

ii. Kampuni ya simu ya Airtel Tanzania imepanga kupeleka huduma ya Wi-Fi katika maeneo **16** kati ya **120** yaliyopendekezwa na Wizara kwa Mwaka 2024/25. Maeneo yatakayofikishiwa huduma ni: Vyuo, Masoko, Hospitali, Vituo vya mabasi na Stesheni za treni ya mwendokasi;

iii. Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika – MISA, imepanga kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano nchini; na

iv. Kushirikiana na Serikali katika kukuza bunifu za TEHAMA na kukuza kampuni changa za TEHAMA.

**SHUKURANI**

***33. Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo wa dhati ninapenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee niwashukuru Mheshimiwa **Maryprisca Winfred Mahundi (Mb.),** Naibu Waziri; **Mohammed Khamis Abdulla,** Katibu Mkuu na **Nicholaus Merinyo Mkapa**, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo katika Wizara, Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia Habari na TEHAMA.

***34. Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue fursa hii kipekee kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta za Habari na Mawasiliano. Washirika hao ni: Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU); Shirika la Umoja wa Posta Duniani (UPU); Shirika la Umoja wa Posta Afrika (PAPU); Benki ya Dunia (WB) kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa (IDA), Ubalozi wa Korea Kusini nchini na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD).

***35. Mheshimiwa Spika,*** ningependa pia kuzishukuru Jumuiya za Kikanda na Kimataifa za Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Ulaya (EU) kwa ushirikiano katika masuala ya Kikanda na Kimataifa yanayohusu Sekta hii. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inachangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia Uchumi wa Kati wa Juu ifikapo Mwaka 2025. Kwa upekee niyatambue makampuni ya mawasiliano ya simu ya Vodacom Tanzania, Airtel Tanzania, Honora Tanzania, Halotel, TISPA na TTCL kwa kusambaza huduma za mawasiliano nchini. Vilevile, napenda kuzitambua taasisi za kifedha ikiwa ni pamoja na benki ya CRDB, NMB, TSA kwa mchango wao katika kukuza bunifu za TEHAMA nchini. Pia napenda kuvishukuru vyombo vya Habari vyote pamoja na Jumuiya zake ikiwemo MOAT, TAMWA, MCT, UTPC, MISA Tan, TADIO, TMF, TEF, JOWUTA, JUMIKITA na Jamii Forums kwa kuendelea kuhabarisha umma. Kwa kumalizia natambua mchango wa wadau wote wa Sekta ikiwemo Kampuni ya Minara Tanzania, Herios Tower, Huawei, Softnet, Telecom Associate, TanzTech pamoja na Raddy Fibre.

**MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MWAKA 2024/25**

***36. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/25, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni mia moja themanini, milioni mia tisa ishirini na sita, mia tano hamsini na saba elfu** kwa mchanganuo ufuatao:-

i. Kiasi cha **Shilingi bilioni thelathini na nane, milioni mia tisa na sita, mia sita sitini na tatu elfu** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni ishirini na nne, milioni mia tisa tisini na saba, mia nne sabini na nne elfu** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi bilioni kumi na tatu, milioni mia tisa na tisa, mia moja themanini na tisa elfu** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

ii. Kiasi cha **Shilingi bilioni mia moja arobaini na mbili, milioni kumi na tisa, mia nane tisini na nne elfu** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni mia moja kumi na sita, milioni mia nne sitini na tisa, mia nane tisini na nne elfu** ni Fedha za Ndani na **Shilingi bilioni ishirini na tano, milioni mia tano hamsini** ni Fedha za Nje.

***37. Mheshimiwa Spika***, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni http://www.mawasiliano.go.tz.

***38. Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.





# Wawili mbaroni tuhuma kukutwa na bunduki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wawili wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kukutwa na bunduki bila kuwa na kibali, huku wakiitumia kwenye uhalifu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Nerbat Mbwiga (33) mkazi wa Ifumbo wilayani Songwe na Isaya Zumba (38) mkazi wa Airport Songwe.

**Jeshi hilo linaendelea na misako ya kuwakamata wahalifu wakiwemo wanaokiuka sheria za usalama barabarani ili kupunguza matukio hayo.**

Kamanda Kuzaga alisema watuhumiwa walikamatwa Mei 11 mwaka huu baada ya kufanyika kwa msako maalumu katika maeneo mbalimbali.

Alisema watuhumiwa hao waliiiba silaha hiyo Aprili 29, 2023 baada ya kuvunja Benki ya Black iliyopo Nzovwe jijini Mbeya.

Alisema kufuatia tukio hilo, Jeshi la Polisi lilifanya ufuatiliaji ambapo Mei 11 lilimkamata Mbwiga katika Kijiji cha Itete Kilichopo Kata ya Isuto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya akiwa na silaha hiyo.

"Mtuhumiwa alikiri kuitumia silaha hiyo katika matukio mbalimbali ya uhalifu kwa kushirikiana na mtuhumiwa mwenzake Zumba, tunaendelea na mahojiano ili kupata mtandao mzima wa watu wanaojihusisha na matukio hayo," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema jeshi hilo litahakikisha linafuatilia na kuwanasa wote wanaoshirikiana na watuhumiwa hao ili kuwafanya wananchi waendelee kufanya shughuli za uzalishaji kwa amani na utulivu.

Aidha, aliwataka vijana wa mkoa huo kutafuta kazi halali za kufanya na kuachana na uhalifu kwa maelezo kuwa njia za mkato za kujipatia kipato hazina nafasi ndani ya mkoa huo.

Pia, aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za viashiria vya uhalifu na wahalifu ili waweze kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kamanda Kuzaga alisema uhalifu ukidhibitiwa vizuri katika mkoa huo kuna uwezekano mkubwa wa kasi ya kukua kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuvutia wawekezaji.

Alisema jeshi hilo linaendelea na misako ya kuwakamata wahalifu wakiwemo wanaokiuka sheria za usalama barabarani ili kupunguza matukio hayo.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (NEC) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela akisisitiza jambo juzi alipozungumza na wajumbe wa Seneti ya Vyuo na Vyuo Vikuu Mkoa wa Mbeya ambapo aliwafundisha mambo mbalimbali yakiwemo ya uongozi na Uchumi. **PICHA:NEBART MSOKWA**

## Wanunuzi tumbaku wanaochezea mizani waonywa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imetahadharisha kampuni za ununuzi wa tumbaku wilayani humo kuacha kuchezea mizani, ikidai kuwa watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mbarak Batenga aliyasema hayo juzi alipozungumza na baadhi ya wakulima waliojitokeza kuuza tumbaku yao katika Chama cha Msingi cha Mtanila wilayani huo ambapo alisema serikali haiwezi kukubali wananchi waumizwe.

Alisema mizani yote inayotumika kwenye ununuzi wa tumbaku na mazao mengine ya wakulima wilayani humo lazima zihakikiwe na Wakala wa Vipimo (WMA) ili kuepuka uhuni unaofanywa na baadhi ya wanunuzi na kusababisha migogoro.

"Mkoa wetu huu wa kitumbaku wa chunya umekuwa ukisifika kwa uzalishaji wa tumbaku bora, wakulima wanatumia gharama zao kuzalisha kuanzia hatua za awali mpaka kwenye mavuno, wengine wanaendesha kilimo hiki kwa mikopo sasa anajitokeza mtu anawaibia, tutashughulika nao," alisema Batenga.

Alisema kampuni itakayobainika ikishiriki kufanya uhuni huo itafungiwa kufanya shughuli hiyo ndani ya wilaya hiyo na wahusika kuchukuliwa hatua zaidi za kisheria ikiwemo kupelekwa mahakamani.

Alisema yapo baadhi ya maeneo nchini yameibuka malalamiko ya wakulima kutokana na uwepo wa mizani ambazo zina Upungufu na hivyo akataka jambo hilo lisitokee kwa wakulima wa zao wilayani humo.

# Wakulima, wafugaji Mbarali wamuita Samia utatuzi mgogoro

**Na Elizabeth John,** MBARALI

WAKULIMA na wafugaji wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wamemuomba Rais Samia Suluhu Hassan kutatua mgogoro wa eneo kati yao na Mamlaka ya Uhifadhi wa Taifa (TANAPA) ili kunusuru madhara yanayojitokeza.

Walieleza ombi hilo wakati wa mkutano maalumu wa hadhara ulilenga kujadili hatma ya maisha ya wakazi wa eneo hilo kufuatia madhira wanayopitia ikiwemo mauaji, mateso na kuporwa mali.

Wamesema hawaitaji eneo la mwekezaji na badala yake wanamuomba Rais Samia Suluhu Hassan awasaidie ili waweze kuachiwa ardhi yao ya asili.

Mmoja wa wakazi hao, Athanas Ngomango alisema: "Leo hii tunanyang'anywa ardhi na wafugaji wananyang'anywa ng'ombe wanaenda kuuzwa alafu wanapoenda kuuza hao ng'ombe wanapigiana simu kwamba fulani leo tumekamata ng'ombe huku njooni mnunue ni kama dili".

Huruma Penya aliiomba serikali kuwasaidia kurudishwa maeneo yao ili kuendelea na shughuli za kiuchumi ikiwemo kusomesha watoto.

"Tunahitaji watusaidie huu mgogoro wa ardhi wa Mbarali uishe ili tuendelee kulima ardhi yetu, tuwe na amani na ardhi yetu na vizazi vinavyokuja na vizazi vinavyoendelea," alisema Penya.

Naye Sayuni Mgaya aliwataka viongozi wa serikali kutochukulia mgogoro huo kama sehemu ya mtaji wa kisiasa badala yake wasimame kati ili kunusuru uhai wa watu na mali zao kwa kutafuta ufumbuzi wa mgogoro huo.

Mkutano huo wa hadhara ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa akiwemo Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Mkoa wa Mbeya, Dickson Kilufi, ambae alisema wameshuhudia matukio ya wafugaji kuuwawa kunyang'anywa mifugo yao na kufilisiwa.

Pia, alikuwepo Mwenyekiti wa Chama cha Democratic Party (DP) Osward Mndeva ambae alisisitiza umoja bila kubaguana kwa misingi ya kisiasa, pindi wanapopigania kudai haki yao

"Usiseme mimi niko CCM, CHADEMA, ACT Wazalendo siyo kwenye ardhi hii," alisema Osward Mndeva.

Kadhalika alisema awali kumekuwepo na matukio ya mauaji, mateso, uporaji mali kupotea tangu mgogoro huo ulipoanza miaka 16 iliyopita.



## Simulizi ya binti mwenye kifafa alivyovuka viunzi

**Na Christina Mwakangale**

ISREY Ayoub (25), ni shujaa wa kifafa. Amefanya mitihani ya taifa mara mbili, kidato cha nne na cha sita, akiwa na hali hiyo. Ndivyo historia ya binti huyo inavyoanza.

Mara kadhaa akiwa pekee yake, shule ya bweni, alikuwa na hali ya kuogofya 'hallucination', hisia zilizomfanya akipita eneo tulivu, ahisi kuna hatari mbele yake.

Isrey, alianza matibabu ya afya ya akili Hospitali ya Taifa ya Akili Mirembe (sasa Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili) mwaka 2016, akiwa kidato cha nne, huku dalili hizo zikianza akiwa kidato cha kwanza.

Binti huyo aliyasema hayo, akifanya mahojiano na Nipashe, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), iliyotaka kufahamu changamoto anazopitia pamoja na matarajio yake, miaka nane tangu abainike anaugua kifafa.

"Kuna changamoto katika jamii, unapewa majina ambayo yanakufanya uhisi vibaya. Mfano kuna siku nilipoteza fahamu nikiwa nje ya nyumbani...kuja kushtuka umezungukwa na watu.

"Unyanyapaa, wengine wanaachika katika ndoa, mtu anashindwa kuwa na mpenzi kutokana ana kifafa," alisema Isrey.

Bingwa Mwandamizi wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka MNH, Dk. Saidi Kuganda, alisema wanaougua kifafa, rekodi ya muda wa kupoteza fahamu kwa wanaougua ugonjwa huo, mara nyingi ni ule ule.

"Huishi kwa masharti fulani fulani, namna ya kulala, yaani ulale upande upi kitandani, hasa usiku, haulali tu ovyo," alisema bingwa huyo ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti cha Chama cha Wataalamu wa Afya ya Akili (MEHATA).

Simulizi kuhusu binti huyo, itaendelea kwenye makala katika gazeti la Nipashe, wiki ijayo.

# Sekta ya uchumi wa buluu kutiliwa mkazo 2024/25

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah amesema serikali inaendelea kuweka mkazo katika uimarishaji wa sekta ya uchumi wa buluu, ili kuhakikisha kunakuwapo na ongezeko la tija kwa wananchi na serikali.

Aliyasema hayo jana wakati akiwalisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya Mwaka 2024/2025 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema tayari kwa mwaka 2023 kuna ongezeko kubwa la kiwango cha uzalishaji wa samaki kilichofikia tani 80,085 wenye thamani ya Sh. Bilioni 569.07 kutoka tani 61,794 (Sh. Bilioni 391.37) mwaka 2022.

"Hili ikiwa ni ongezeko la asilimia 29.5. Vilevile, uzalishaji wa mwani umeongezeka kutoka tani 12,594 mwaka 2022 hadi kufikia tani 16,653 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 32.2." alisema Hemed.

Aidha, alisema serikali imeendelea kuchukua jitihada ya kuweka mifumo ya kitaasisi ili kuifanya sekta hiyo kuendelea kuwa tegemeo katika kukuza uchumi wa wananchi na taifa.

Alisema miongoni mwa jitihada hizo ni kuwa na sera na sheria ambazo zitatumika katika utekelezaji na uendelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu, ikiwemo Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini ambayo tayari imeshasainiwa na Rais Hussein Ali Mwinyi.

Akizungumzia biashara, Hemed alisema serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kununua tani 4,380 za karafuu kavu kwa Sh. bilioni 60.4, kwamba hadi kufikia Machi, 2024 tani za karafuu kavu 3,298.8 zimenunuliwa kutoka kwa wakulima kwa Sh. bilioni 47.5.

Aidha, alisema serikali ilipanga kununua tani 786 za makonyo kwa Sh. bilioni 1.17, kwamba hadi kufikia Machi, 2024 serikali ilinunua tani 627.6 kwa gharama ya Sh. milioni 941.4.

Hemed alisema serikali pia imeuza nje ya nchi tani 3,190 za karafuu na tani 694 za makonyo.

Alisema serikali katika kuendelea kuitangaza nchi kibiashara imejenga Kituo cha Maonesho ya Biashara eneo la Dimani, Wilaya ya Magharibi B.

Alisema ujenzi wa kituo hicho kinajumuisha ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua zaidi ya watu 1,500 na mabanda ya maonesho yenye uwezo wa kuchukua wafanyabiashara zaidi ya 650, hivi sasa umekamilika kwa asilimia 80.

Alisema serikali inaendelea kuimarisha mazingira ya biashara pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda ili kusaidia kuongezeka kwa bidhaa na kukua kwa uchumi wa nchi.

Hivyo, aliwataka wananchi na wafanyabiashara kutumia fursa zilizopo za biashara kwa lengo la kuendeleza dhima ya serikali ya kupanua wigo wa biashara pamoja na kupata ajira kupitia sekta ya viwanda na biashara.



Mbuzi wakirandaranda mitaani eneo la Mbezi Kwa Yusuph Dar es Salaam juzi, bila kuwa na mchungaji, kitendo ambacho kinaweza kuhatarisha usalama wao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali: Tunatambua mchango wa wadau katika kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema serikali inathamini juhudi za washirika wa maendeleo katika kuunga mkono katika kuimarisha sekta ya kilimo nchini.

Aliyasema hayo juzi visiwani hapa wakati wa uzinduzi wa utoaji wa matokeo ya uchunguzi wa sampuli za udongo kwa wakulima wa Zanzibar uliofanyika katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) Kizimbani Wilaya ya magharibi 'A', Unguja.

Alisema udongo ni muhimili mkubwa wenye uzalishaji wa kilimo cha kujikimu kimaisha na kuchangia pato la taifa, hivyo ni vyema utunzwe na kuhifadhiwa kuhakikisha kilimo kinakua chenye tija na endelevu.

Aidha, alisema kuwa Zanzibar ina udogo wa ardhi kwa maeneo ya uzalishaji na kila mtu anahitaji kujikimu kimaisha kwa kilimo.

Alisema ndiyo maana serikali kupitia washirika wa maendeleo iliona ipo haja ya kufanya uchunguzi wa afya ya udongo katika visiwa vya Unguja na Pemba kubaini upungufu wa wakulima ambayo itakua ni fursa kwao juu ya uzalishaji.

Alisema ni wajibu wa kila mkulima kufanya uchunguzi wa udongo ili kujua upungufu uliopo na itasaidia kujua hadhi ya udongo na aina gani ya virutubisho vinavyohitajika kuongezwa.

"Nawaomba wakulima mshirikiane na wataalamu wetu ili muweze kuongeza kipato cha kujikimu kimaisha sambamba na kuwa na tabia ya kuchunguza afya za udongo kila baada ya muda, ili kuifanya ardhi iendelee kuzalisha mazao bora", alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ali Khamis Juma, aliitaka taasisi za kilimo na wakulima kuendelea kupima afya ya udongo ili kupata uhakika wa uzalishaji wa mazao mengi, akisema hatua hiyo itakua ni moja katika mkakati wa kusaidia kwenda katika kilimo cha kibiashara na siyo kwa kujikimu peke yake.

Mkurugenzi Mkuu wa ZARI, Dk. Mohamed Dhamir Kombo, alisema mwaka jana walifanya makubaliano ya ushirikiano na World Vegetable Center kufanya kazi pamoja kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao hasa ya mboga.

Alisema kutokana na changamoto zilizopo za wakulima husussani katika suala la mbegu na mbolea ndiyo maana wakaona ipo haja ya kuwasaidia wakulima katika kuchunguza afya ya udongo, ili wakulima wapate mazao mazuri na yenye kuleta tija.

Ofisa Mradi wa World Vegetable Centre, Nickson Mlowe, aliwataka wakulima kuwa mabalozi wa kuhamasisha wenzao kupima afya ya udongo na matokeo hayo yatakayopatikana itakuwa ni chachu ya kupeleka mbele kilimo bora.

## HABARI KIMATAIFA

# Misri, Israel zavutana kufungwa kwa mpaka

**CAIRO, Misri**

NCHI za Israel na Misri ziko kwenye mvutano kuhusu mpaka wa Rafah, zikilaumiana baada ya kuendelea kufungwa wakati ikishuhudiwa hali mbaya ikizidi kuhatarisha maisha ya binadamu Ukanda wa Gaza.

Vikosi vya Israel vimeudhibiti upande wa pili wa mpaka huo siku ya Jumanne.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Israel, Israel Katz, aliziambia nchi za Uingereza na Ujerumani kwamba kuna haja ya kushawishi Misri kufungua tena mpaka huo.

Hata hivyo, Misri ilisema kuwa operesheni za kijeshi za Israel katika eneo hilo zinazuia misaada kuingia ndani ya gaza.

Uongozi wa Misiri ulieleza kwamba Israel inajaribu kuelekeza lawama upande wao kuhusu kuzuiliwa kwa misaada hiyo, jambo ambalo sio kweli.

Waziri Katz alisema kundi la wapiganaji la Palestina Hamas, haliwezi tena kudhibiti mpaka wa Rafah, kwa sababu hawawezi kuvumilia hofu ya kiusalama.

„Ulimwengu unaweka jukumu la hali ya kibinadamu kwa Israel, lakini umuhimu wa kuzuia janga la kibinadamu huko Gaza sasa liko mikononi mwa marafiki zetu wa Misri, alisema Katz kupitia mtandao wa X.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Misri, Sameh Shoukry, alijibu haraka lawama hizo kwa kueleza kwamba Israel inahusika na mgogoro wa kibinadamu ndani ya Gaza kutokana na hatua za jeshi la Israel katika eneo la Rafah.

Misri imekuwa moja ya wapatanishi katika mazungumzo yaliyokwama ya kusitisha mapigano, lakini uhusiano wake na Israel umekuwa mbaya tangu Israel ilipoteka upande wa pili wa mpaka wa Rafah, Mei 7, mwaka huu.

Tangu eneo la Rafah kuvamiwa na vikosi vya Israel, Wapalestina 450,000 wamekimbia wiki iliyopita na kwenda maeneo mengine ya Ukanda wa Gaza.

Vifaru vya Israel vinaripotiwa kuingia ndani zaidi katika mji huo ulioko kaskazini mwa mpaka huo.

Wakati huo huo, serikali ya Marekani imeliambia bunge la Congress kuwa inataka kupeleka silaha nchini Israel zenye gharama ya dola bilioni moja.

Kulingana na shirika la habari la Reuters, kifurushi hicho kitajumuisha silaha, chokaa na magari ya kivita.

Mpango huo, uliothibitishwa na kupatiwa CBS, lazima uidhinishwe na wabunge.

Wiki iliyopita Rais Joe Biden, alisema kuwa atasitisha usafirishaji wa silaha kwenda Israel ikiwa itaanzisha uvamizi kamili katika mji wa Rafah.

Rais Biden alisema alichelewesha usafirishaji wa mabomu yenye thamani ya dola 2,000 kwenda Israel kwa sababu yanaweza kutumika katika operesheni hiyo ya ardhini.

Alipoulizwa na CNN kuhusu ucheleweshaji huo, kiongozi huyo alisema kuwa raia wameuawa Gaza kutokana na mabomu hayo.

Msaada huo ni wa kwanza tangu utawala wa Biden kusitisha uhamishaji wa silaha kwenda Israel wiki iliyopita.

Siku ya Ijumaa, ripoti ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani iligundua kuwa baadhi ya silaha za Marekani zilizotolewa kwa Israel huenda zilitumika kinyume na sheria za kimataifa.

Ingawa ripoti hiyo ilikuwa ni karipio la wazi la baadhi ya operesheni za Israel katika Ukanda wa Gaza, ilimaliza kwa kusema kwamba kampeni ya Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) ilikiuka sheria za kimataifa.

***BBC***

# Ali Bongo agoma kula

**LIBREVILLE, Gabon**



RAIS wa zamani wa Gabon, Ali Bongo, ambaye aliyeondolewa madarakani na jeshi na wanawe wawili wamegoma kula na wakilalamika kufanyiwa vitendo vya kikatili.

Mawakili wa familia hiyo walisema kuwa kiongozi huyo na watoto wake Jalil na Bilal wameitisha mgomo huo kutokana na serikali ya kijeshi kuwapa mateso wakiwa kwenye kizuizi cha nyumbani.

Bongo aliondolewa madarakani katika mapinduzi ya kijeshi yaliyofanyika mwezi Agosti mwaka jana, muda mfupi baada ya kushinda kura ya urais iliyoibua mgogoro wa kisiasa.

Baada ya mapinduzi hayo, Bongo na familia yake walizuiwa kwenye makazi yake yaliyoko katika mji mkuu, Libreville.

Serikali hiyo pia iliwashikilia mkewe Sylvia Bongo na mwanawe mkubwa Noureddin, wakisubiri kufikishwa mahakamani kwa tuhuma za rushwa.

Katika taarifa ya mawakili wao walidai kuwa Noureddin na Sylvia walipigwa na kunyongwa wakiwa kizuizini.

Pia wanadai kuwa Noureddin aliteswa, kuchapwa viboko na hata kupigwa na shoti ya umeme.

Rais huyo aliyeondolewa madarakani, mwenye umri wa miaka 64, aliongoza nchi hiyo yenye utajiri mkubwa wa mafuta tangu 2009 aliporithi kutoka kwa baba yake ambaye amekuwa madarakani kwa zaidi ya miaka 40.

Mawakili wa familia hiyo walisema wamewasilisha malalamiko katika mahakama ya Paris, wiki moja kabla ya kiongozi wa serikali ya Gabon, Brice Oligui Nguema kufanya ziara nchini humo.

***BBC***

# Kiongozi upinzani azuiwa kugombea urais Rwanda

**KIGALI, Rwanda**

MAHAKAMA ya nchini Rwanda imekataa rufani ya mwanasiasa wa upinzani, Bernard Ntaganda (55) ambaye alipinga hukumu ya awali ya kuzuiwa kugombea nafasi ya urais.

Ntaganda, ambaye anatoa upinzani mkali kwa Rais Paul Kagame, aliiomba Mahakama Kuu kubatilisha hukumu iliyotolewa muongo mmoja uliopita ambayo imemzuia kushiriki uchaguzi mkuu utakaofanywa Julai mwaka huu. Majaji watatu kwa pamoja walikataa rufani ya Ntaganda, wakisema kwamba mwanasiasa huyo hakulipa kiasi cha faranga 106,000 za Rwanda kama ada ya kesi ya awali.

„Mahakama Kuu imehitimisha kuwa Bernard Ntaganda alishindwa kufuata sheria inayowataka watu binafsi kutaka kubatilishwa kwa hukumu zao, na hivyo mahakama inakataa rufani yake," ilisema hukumu hiyo.

Ntaganda, ambaye ni wakili na mwanzilishi wa chama cha PS-Imberakuri, alieleza kuwa ana uthibitisho wa malipo ya ada hizo na hashangazwi na uamuzi huo wa mahakama.

Kiongozi huyo ni wa pili wa upinzani kuzuiwa kushiriki katika uchaguzi huo dhidi ya Paul Kagame. Mwezi Machi, mpinzani mwingine wa muda mrefu, Victoire Ingabire, alifungwa jela mwaka 2013 na kumzuia kugombea.

***RFI***


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTLINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UKONGA | GEORGE JAPHET NDENGA | NYUMBA | GEORGE JAPHET NDENGA | KINYEREZI | 21/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ABDULHMAN RAJABU MAHABA | NYUMBA | ABDULHMAN RAJABU MAHABA | ZINGIZIWA | 24/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | MAX AYUBU MBONYE | NYUMBA | MAX AYUBU MBONYE | YONGWE-CHANIKA | 24/05/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | JUMA NURU MUSHI | NYUMBA | JUMA NURU MUSHI | MBAGALA | 24/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | RAHABU ERASTO MESSO | NYUMBA | RAHABU ERASTO MESSO | KWEMBE-UBUNGO | 21/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | NYUMBA | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | TEGETA 'A' - GOBA | 31/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ALOYCE JOHN KAZIMBAYA | NYUMBA | ALOYCE JOHN KAZIMBAYA | MADALE NYAKASANGWE | 07/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | JONATHAN ZAWADI MHANDO | NYUMBA | JONATHAN ZAWADI MHANDO | MBEZI MSAKUZI | 23/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHACHA ITEMBE NYAMAISA | NYUMBA | SHAABAN SHILLINDE BULILO | NYAMHONGOLO-MWANZA | 31/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | FAUSTINE KISYERI MAIHA | NYUMBA | DEUSDEDIT NYANDA MIKOMANGWA | NYAMANORO - MWANZA | 31/05/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| AGGREY | INNOCENT DIDAS MUMBURI | NYUMBA | KHADIJA SEIF SINKAMBA | VINGUNGUTI- ILALA | 23/05/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | RAJABU MOHAMED MUOMBWA | NYUMBA | RAJABU MOHAMED MUOMBWA | YANGEYANGE-MSONGOLA | 29/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | ANOLD ANTONY MIKA | NYUMBA | ANOLD ANTHONY MICHAEL | NKUHUNGU DODOMA | 20/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0767808848/0765999000/00714939933/0754497396**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# KOCHA PRISONS AWASHANGAA WACHEZAJI

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa klabu ya Tanzania Prisons, Ahmed Ally amesema katika michezo ya hivi karibuni wachezaji wake hawajacheza kwenye ubora wao na kupelekea kucheza michezo minne bila ushindi wowote.

Kocha huyo amesema wana uwezo wa kumaliza ndani ya 'Top 4' kama watapambana na kupata ushindi kwenye michezo ijayo na kuomba wapinzani wao kwenye nafasi hiyo kuteleza katika michezo yao.

Alisema michezo hiyo minne waliyocheza bila kupata ushindi imewafanya kuwa kwenye nafasi waliyopo sasa katika msimamo wa Ligi Kuu.

"Tumekuwa tukicheza kama vile tumemaliza msimu, sijui nini kimetokea kwa wachezaji wangu, lakini tunapaswa kuamka na kupambana kwenye michezo iliyobakia ili tupate ushindi na kuangalia kama tunaweza kumaliza kwenye nafasi ya nne," alisema Ally.

Alisema michezo hiyo mitatu iliyobakia ni muhimu sana kwao na ameongea na wachezaji wake kuongeza umakini na kujituma ili wamalize na ushindi Ligi kuu.

"Nafahamu haitakuwa michezo rahisi, kila timu inahitaji ushindi hasa katika mechi hizi zilizobakia ili kujua mwishoni mwa msimu watakuwa kwenye nafasi gani, lazima tuwe makini katika kila mchezo na kuongeza umakini," alisema.

Tanzania Prisons inashika nafasi ya tanokwenye msimamo wa Ligi ikiwa na pointi 33 baada ya kucheza michezo 27 mpaka sasa ikizidiwa kwa pointi tano ya Coastal Union inayoshika nafasi ya nne, timu hizo zote zimecheza michezo sawa.

Pia Maafande hao wa Magereza wanalingana pointi na KMC wanaoshika nafasi ya sita huku wote wakilingana michezo, hata hivyo Tanzania Prisons wapo juu kutokana na uwiano mzuri wa magoli ya kufunga na kufungwa.



Wachezaji wa timu ya Kitunda FC, Mwita Samwel (kushoto) na Shabani Njiti, wakiwania mpira wakati wa mazoezi ya timu hiyo katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DC aandaa mikakati kuinusuru Geita FC

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Geita, Hashim Komba, amejitokeza na kueleza mikakati ya Uongozi wa Halmashauri ya Mji huo kuinusuru timu ya Geita Gold isishuke daraja.

Akizungumza wilayani humo, Mkuu huyo amesema kuanzia sasa watashirikiana na uongozi wa klabu hiyo, benchi la ufundi ili kuhakikisha mahitaji yote yanayohitajika yanapatikana ili timu hiyo iweze kuendelea kuwepo Ligi Kuu.

"Tuna michezo mitatu mkononi, tunajua kwamba ni michezo migumu, tunatacheza dhidi ya Simba, Singida Fountain Gate na Azam FC, wajibu wetu kama viongozi ni kushirikiana na uongozi wa klabu na benchi la ufundi, tuhakikishe mahitaji yote yanayohitajika yanapatikana ili timu yetu iweze kuendelea kuwepo Ligi Kuu, haitakuwa jambo zuri timu ishuke" alisema Komba.

Alisema hawawezi kuacha timu hiyo ikishuka daraja kwa sababu ni alama na fahari kwa wilaya ya Geita na Mkoa kwa ujumla wake.

"Geita Gold ni fahari yetu, ni timu ambayo ni alama kwa wilaya yetu kwa hiyo kazi kubwa tuliyonayo kama viongozi ni kuwaleta watu wote pamoja katika hatua hizi za mwisho ili tuweze kuhakikisha tunabakia," alisema.

Timu hiyo ipo kwenye nafasi ya 15 katika msimamo wa Ligi Kuu, imecheza michezo 27, imeshinda michezo mitano, imetoka sare michezo 10 na kufungwa michezo 12 huku ikijikusanyia pointi 25.

Geita Gold imebakisha mechi tatu, ambapo Mei 21 itacheza na Simba Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, baada ya hapo itaumana na Singida Fountain Gate kwenye uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza na baadae itamaliza ligi kwa kucheza na dhidi ya Azam FC, Mei 28.

# Tabora United yaita mashabiki uwanjani

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tabora United, imesema ili kujiweka katika mazingira mazuri ya Ligi Kuu, ni lazima iifunge Ihefu FC katika mechi itakayochezwa Jumatano ijayo kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, hivyo imewaomba mashabiki wake kujitokeza kwa wingi ili kusaidia kufanikisha mpango wao wa kuondoka na pointi tatu muhimu.

Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mrundi Masoud Djuma, amesema itakuwa mechi ya kufa na kupona kwani lazima wapate pointi tatu, vinginevyo hali itakuwa mbaya kwao.

"Tukitaka kunusurika ni lazima tupate pointi tatu, hakuna kutafuta sare, kwa sababu kilichobaki sasa si kuangalia mwenzako amepoteza, ni wewe kushinda tu.

"Tukipata pointi tatu tutapata nguvu ya kusaka ushindi katika mechi zinazobakia," alisema kocha huyo wa zamani wa Simba.

Pia, amesema amefurahi kuona kwa mara ya kwanza mshikamano uliopo kwa wakazi wa Tabora ambao wameonekana kuiunga mkono katika kipindi hiki tofauti na ilivyokuwa awali.

"Nimeona kwa mara ya kwanza sapoti kubwa katika mchezo dhidi ya Mashujaa, watu hawakuizomea timu, kila mtu alishangilia na tulipopata ushindi walitupongeza, tukiendelea hivi nina imani tutashinda mechi zinazofuata na kubaki Ligi Kuu," alisema.

Aidha, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Christina Mwagala, alikiri kuwa timu yao inakabiliwa na mchezo mgumu ndiyo maana wameanza maandalizi mapema ya mchezo huo huku akiwaomba mashabiki wa timu hiyo wasali na kuiombea timu yao.

"Tuna mchezo mgumu dhidi ya Ihefu FC, ndiyo maana tumeanza maandalizi mapema kwa ajili ya kuhakikisha pointi tatu muhimu zinabaki hapa kwenye uwanja wetu wa Ali Hassan Mwinyi. Jamani mashabiki tunaomba tuiombee timu yetu, mwenye kuomba aombe, mwenye kusali asali," alisema Christina.

Timu hiyo ipo katika nafasi ya 14, ikiwa na pointi 26, ikibakisha michezo mitatu ambayo ni dhidi ya Ihefu, Yanga, mechi itakayochezwa Mei 25, Uwanja wa Azam Complex, na Namungo, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi, Mei 28.

## ZISIKUPITE

### WATKINS ATAKIWA MAN
MANCHESTER United inataka kumsajili mshambuliaji wa England, Ollie Watkins kutoka Aston Villa kwani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 analingana na wasifu wa mchezaji ambaye wanataka kumsajili. ***(Talksport)***

### SESKO ATAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal inafikiria kuwasilisha dau la pauni milioni 60 kumnunua mshambuliaji wa RB Leipzig raia wa Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 20. ***(Telegraph)***

### SALAH, BECKER WASAKWA
MSHAMBULIAJI wa Liverpool na timu ya taifa ya Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31 na kipa wa Brazil Alisson Becker mwenye miaka 31, ni miongoni mwa wachezaji wanaosakwa na klabu za Saudi Pro League msimu huu. ***(Guardian)***

### TEN HAG NA MAN UNITED
NAFASI ya Erik ten Hag kubaki kuwa kocha wa Manchester United inalegalega, huku mustakabali wa Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 54 ikitarajiwa kuamuliwa baada ya fainali ya Kombe la FA mnamo Mei 25. ***(Guardian)***

### THOMAS TUCHEL KUBAKIZWA
THOMAS Tuchel, ambaye yuko kwenye orodha fupi ya Manchester United ya makocha wanaotarajiwa kuchukua nafasi ya Erik Ten Hag, yuko kwenye mazungumzo ya kusalia Bayern Munich, baada ya kupanga kuondoka mwishoni mwa msimu huu. ***(Times)***

### ESTEVAO ANUKIA CHELSEA
CHELSEA imeandaa ofa mpya kwa winga wa Palmeiras, Willian Estevao baada ya kuafikiana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 17 wiki iliyopita. ***(Fabrizio Romano)***

### VILLA KUUZA MMOJA
LICHA ya kufuzu kwa Ligi ya mabingwa Ulaya, Aston Villa italazimika kuuza angalau mchezaji mmoja kwa ada kubwa msimu huu wa joto ili kuzingatia Kanuni za Faida na Uendelevu za Ligi Kuu. ***(Sun)***

### MOURINHO ANYATIWA SAUDIA
KOCHA wa zamani wa Chelsea, Manchester United na Tottenham Hotspur, Jose Mourinho ananyatiwa na klabu ya Al-Qadsiah ya Saudi Arabia. ***(Mail)***

### CHELSEA KULIPWA
CHELSEA itapata nyongeza ya pauni milioni 5 chini ya masharti ya uhamisho wa Eden Hazard kwenda Real Madrid wa mwaka 2019, baada ya timu hiyo ya Hispania kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya - licha ya mshambuliaji huyo wa zamani wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 33 kustaafu miezi saba iliyopita. ***(Telegraph)***

### THURAM KUTUA LIVERPOOL
LIVERPOOL imepewa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Nice na Ufaransa, Khephren Thuram mwenye umri wa miaka 23 kwa pauni milioni 13 msimu huu. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG ASISITIZA FERNANDEZ ATABAKI MANCHESTER UNITED

Kocha huyo alimuhakikishia nahodha wa United kuwa wanataka kumbakisha baada ya mreno huyo kusema….

**MANCHESTER, England**

KOCHA Erik ten Hag amemuhakikishia kiungo wake Bruno Fernandes kwamba Manchester United wanataka kumbakiza msimu huu wa majira ya joto baada mreno huyo kusema kuwa atasalia tu ikiwa anahisi kuhitajika Old Trafford.

Fernandes amekuwa akihusishwa na kutaka kuhama mwishoni mwa msimu huu na ESPN iliripoti Jumatano kwamba klabu ya ‚Saudi Pro League‘ ya Al Nassr ni moja ya timu zinazovutiwa nae.

Akizungumza baada ya ushindi wa 3-2 wa United dhidi ya Newcastle United Jumatano usiku, Fernandes alisema ataondoka ikiwa hatatakiwa.

Lakini akijibu maoni hayo, Ten Hag alimwambia Fernandes kuwa ni sehemu ya mipango ya klabu kwa siku zijazo.

„Klabu inataka kumbakisha Bruno, hakuna swali nadhani,“ alisema Ten Hag.

„Lazima nione mahojiano. Ninavyofahamu na kila ninachofahamu kutoka kwake, anaipenda Manchester United.

„Anawapenda mashabiki na anapenda kuichezea Manchester United. Hivyo ndivyo ninavyojua. Unaona huwa anatoa ubora wake. Ni mfano.“

Fernandes ana mkataba hadi mwaka 2026, lakini hali ya kifedha ya United inamaanisha kwamba ofa kubwa kwa karibu mchezaji yeyote itabidi kuzingatiwa.

Klabu nyingi kutoka barani Ulaya na Saudia zimeonyesha nia ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 na kuuliza kuhusu hatma yake baada ya ushindi dhidi ya Newcastle, alionekana kutumia nafasi hiyo kutuma ujumbe kwa mabosi wa klabu hiyo.

„Klabu inahitaji kunihitaji,“ Fernandes aliambia Sky Sports.

„Ninahisi klabu inataka niwe sehemu ya siku zijazo. Kama nilivyosema siku zote, sitaki kuwa mchezaji ambaye klabu haitaki kuwa naye.

„Ikiwa kwa sababu fulani klabu hainitaki, nitakwenda.“

Ushindi wa juzi unakuja kama ahueni kwa United wakati wa msimu ambao wako mbioni kuwa na mwisho mbaya zaidi wa Ligi Kuu ya England lakini ushindi wa Chelsea dhidi ya Brighton bado unawaacha vijana hao wa Ten Hag nje ya nafasi za kucheza Ulaya kuelekea siku ya mwisho Jumapili.

United bado wana nafasi moja ya kutwaa taji watakapomenyana na Manchester City kwenye fainali ya Kombe la FA mnamo Mei 25.

# Xavi aeleza sababu kutomtumia Roque

**BARCELONA, Hispania**

XAVI amekiri kwamba haukuwa mpango wa Vitor Roque kujiunga na Barcelona wakati alipofanya hivyo majira ya baridi, baada ya kuchagua kutomtumia mshambuliaji huyo wa Brazil kwa mwezi mmoja uliopita.

Mkataba wa Roque uliofikiwa na Athletico Paranaense hatimaye unaweza kujumlisha euro milioni 61, lakini miezi yake ya kwanza nchini Hispania imekuwa migumu kwake.

Uhamisho huo ulikubaliwa katika msimu wa joto wa 2023 kwa nia ya kwamba Roque anaweza kuungana na Wakatalunya mwaka mmoja baadaye. Lakini tarehe hiyo ilisogezwa mbele katikati ya msimu huu.

"Nia haikuwa Vitor Roque kuja Desemba," alieleza Xavi akiwaambia waandishi wa habari.

"Mpango ulikuwa kwamba abaki Brazil na kuendelea kukua. Chaguo lilifunguliwa na majeraha ya Gavi na Alejandro Balde."

Roque alifunga mfululizo katika mechi alizotokea benchi dhidi ya Osasuna na Alaves ndani ya wiki chache baada ya kuwasili.

Lakini pia ameanza mara mbili pekee katika michuano yote, hakushiriki kabisa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya na alikuwa mchezaji wa akiba ambaye hatumiwi katika mechi nne zilizopita za LaLiga za Barca.

Lakini wakati Roque angeweza kusalia Brazil, ambapo aliifungia Athletico mara 21 katika mashindano yote mnamo 2023, Barca waliona ni bora kuwa naye angalau afanye nao mazoezi hata kama muda halisi wa mchezo ungekuwa mdogo.

"Kwa mazoezi yake, tuliamini ni bora zaidi," kocha huyo alieleza.

"Kuna mjadala ambao kwangu hauna maana yoyote. Ni mchezaji wa mazoezini. Kuna wanasoka ambao wako mbele yake, ndivyo ninavyoelewa. Ametumia maisha yake yote na wanasoka chipukizi," Xavi aliongeza.

Lakini kuachwa kwenye kivuli haijapokelewa vyema na kambi ya mchezaji huyo. Andre Cury anayemwakilisha Roque mapema mwezi huu, alitishia kumtafutia mteja wake klabu mpya ikiwa muda zaidi wa kucheza hautatolewa.





# BAYERN KUMSHAWISHI KOCHA TUCHEL KUBAKI

**MUNICH, Ujerumani**

BAADA ya kukataliwa na makocha mbalimbali, Bayern Munich imeripotiwa kufikiria upya kuondoka kwa Thomas Tuchel kama kocha na kutafuta suluhu ya kumshawishi kubaki.

Tuchel anatarajiwa kuondoka mwishoni mwa msimu huu kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa na klabu hiyo Februari.

Lakini kupata mrithi ni vigumu kuliko ilivyotarajiwa kwa Bayern.

Vyombo vya habari vya Ujerumani vya Kicker, jarida la Bild, na Sky TV vyote viliripoti kwamba, wakurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Max Eberl na Christoph Freund walikuwa wakijadiliana na Tuchel ili kutengua uamuzi wao wa makubaliano ya pamoja wa kumuachia aondoke.

Tuchel alishutumiwa vikali na rais wa heshima wa Bayern, Uli Hoeness kabla ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid.

Tuchel angetaka kuongezewa mkataba wake wa awali, ambao ulitarajiwa kumalizika hadi 2025.

Lakini Sky iliripoti kwamba kocha huyo mwenye umri wa miaka 50 yuko tayari kwa wazo la kubakia.

Bild ilichapisha picha Jumatano zikimuonesha wakala wa Tuchel, Olaf Meinking akizungumza na Freund na mwenyekiti wa Bayern, Jan-Christian Dreesen katika ofisi za klabu hiyo.

Wachezaji wa Bayern pia wangependelea Tuchel abaki. Wachezaji wa kimataifa wa Ujerumani, Thomas Müller na Manuel Neuer wameripotiwa kuzungumza kwa niaba yake, huku wachezaji wa England, Harry Kane na Eric Dier pia wanataka abaki.

Mashabiki wengi wa Bayern pia walitia saini ombi la kuitaka klabu hiyo kumbakisha Tuchel.

# Mafuriko yasimamisha ligi Brazil

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

SHIRIKISHO la soka la Brazil limesimamisha mizunguko miwili ijayo ya ligi yake Kuu kwa sababu ya mafuriko makubwa kusini mwa nchi hiyo.

Hatua hiyo imekuja baada ya ombi la kusitishwa kwa klabu 15 kati ya 20 za ligi kuu.

Jimbo la Rio Grande do Sul lipo chini ya maji.

Wapinzani wenye maskani yake Porto Alegre, Gremio na Internacional, na klabu ya mashambani Juventude zote ziko katika daraja la kwanza la Brazil.

Mamlaka inasema takriban watu 149 wamefariki kutokana na mafuriko na wengine 108 hawajulikani walipo. Zaidi ya watu 620,000 wamekimbia makazi yao.

Iwapo hali itaruhusu katika eneo la kusini mwa Brazil, ligi hiyo itaendelea katika raundi ya tisa mnamo Juni 1. Raundi ya saba na ya nane itaratibiwa upya.

"Hatuwezi kusahau kwamba michezo na jamii vinaungana mkono, na hatuwezi kutengana katika wakati mgumu kama huu kwa watu wa Brazil," shirikisho la soka la nchi hiyo lilisema katika taarifa yake.

Liliongeza kusimamishwa kwa mechi za mgawanyiko wa ligi kuu hadi Mei 27 pamoja na mashindano mengine.

Waziri wa michezo wa Brazil, André Fufuca aliomba hatua hiyo hiyo siku ya Ijumaa, na kuipanua kwa mashindano yote ya kitaifa, kwa wanaume, wanawake na chini ya miaka 20.

Shirikisho la soka la Brazil lilikuwa tayari limekubali kusimamisha kwa siku 20 shughuli zote za soka katika jimbo hilo la kusini, ambalo linapakana na Uruguay na Argentina.

Shirikisho la soka la Amerika Kusini, CONMEBOL pia lilisimamisha mechi mbili za ligi ya mabingwa wa Bara hilo katika eneo hilo.

Wakati eneo la Beira-Rio inapotoka Internacional haijafurika tena, Arena do Gremio imesalia chini ya maji katika mji mkuu wa jimbo la Porto Alegre.

Uwanja wa Juventude wa Alfredo Jaconi ulio nje kidogo ya jiji la Caxias do Sul haukuathiriwa sana.

Viwanja vya ndege huko Porto Alegre na Caxias do Sul vimefungwa, usambazaji wa maji bado ni mdogo na hoteli zimejaa.

Klabu zote tatu kutoka Rio Grande do Sul mechi zao za raundi ya tano ya ligi ya Brazil zilisimamishwa, wikendi hiyo hiyo mafuriko yalianza.

Internacional wako katika nafasi ya 10, Gremio wako nafasi ya 12 na Juventude wapo nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi hiyo.

HABARI MICHEZO

# WACHEZAJI COASTAL UNION WAZUIWA KUTUMIA SIMU

Na Saada Akida

KUELEKEA katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho (FA)dhidi ya Azam FC, uongozi wa klabu ya Coastal Union umewapiga marufuku wachezaji wao kutumia simu za mkononi hadi hapo mchezo huo utakapochezwa na kumalizika.

Klabu hiyo imesema lengo la kufanya hivyo ni kuwataka wachezaji kuwa makini na kutuliza akili zao kuelekea mchezo huo utakaochezwa kesho, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Imeelezwa kuwa viongozi wamefanya kikao na wachezaji pamoja na benchi la ufundi kwa lengo ya kuweka mikakati ya pamoja kuelekea mchezo huo na nyota hao kutakiwa kutumia muda mwingi kupumzika na kuufikiria mchezo huo.

Nipashe lilimtafuta Ofisa habari wa Coastal Union, Abass Elsabri ambaye alisema wana kibarua kigumu mbele yao cha mchezo huo wa nusu fainali, wachezaji wanatakiwa kuwa makini na kutuliza akili zao kuelekea mechi hiyo.

Alisema mikakati yao kuelekea mchezo huo ilianzia katika mchezo uliopita wa Ligi Kuu waliocheza ugenini dhidi ya Geita Gold FC ambao walifanikiwa kupata pointi moja sasa wanaelekeza nguvu kwenye mechi ya nusu fainali dhidi ya Azam FC.

"Ni kweli kwa sasa wachezaji wanatakiwa kutulia na kupata muda wa kujiandaa kwa mechi yetu ngumu dhidi ya Azam FC, sasa hivi huwezi kuona nyota wetu wakiwa katika mitandao, wanapata muda wa kupumzika na kujiandaa kuelekea mchezo huo," alisema Ofisa habari huyo.

Aliongeza kuwa malengo yao msimu huu ni kuhakikisha wanafanikiwa kushinda mchezo huo na kucheza fainali ya michuano hiyo na ikiwezekana kutwaa ubingwa na kwenda kushiriki michuano ya kimataifa.

# Waziri Mkuu kufunga Baraza la michezo Majeshi duniani

Na Shufaa Lyimo

WAZIRI Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, leo anatarajiwa kufunga Mkutano Mkuu wa 79 wa Baraza la Mashirikisho ya Michezo ya Majeshi Duniani kwenye Hoteli ya Rotana, Dar es Salaam.

Mkutano huo ulifunguliwa Mei 14 na Makamu wa Rais Dk Phillip Mpango, ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Tanzania kwa mwaka huu wamekuwa wenyeji wa mkutano huo kwa mara ya pili ambapo kwa mara ya kwanza mkutano huo ulifanyika nchini mwaka 1991.

Mkutano huo unahudhuriwa na washiriki zaidi ya 200 kutoka Mataifa wanachama 82 kati ya 140.

Kabla ya kufunga mkutano huo leo, jana Baraza hilo lilitembelea kituo cha vijana cha michezo kilichopo kwenye kambi ya Jeshi ya Twalipo Kurasini.

Akizungumza jana, Rais wa Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (CISM), Kanali Nilron Rolim amewasisitiza wachezaji kuongeza juhudi ili waweze kufika mbali kupitia michezo ya Majeshi.

„Mchezaji mzuri ni yule ambaye pia anafanya vizuri katika masomo yake pamoja na kuwa na nidhamu nzuri muda wote, naamini hapo baadae mtapata mafanikio kupitia michezo hii, alisema Rolim.

Naye Meja Jenerali Dkt Gabriel Mhize ambaye ni Mkuu wa Hospitali ya Lugalo, alisema anashukuru kwa ushirikiano mkubwa alioupata kutoka kwa wageni wao ambao anaamini watafuata yale waliyojadiliana kwenye mkutano huo.





Beki wa Azam FC, Nathaniel Chilambo akisaini mkataba mpya juzi wa kuendelea kuitumikia timu hiyo kwa miaka miwili zaidi. **PICHA: BINZUBEIRY**

## Simba kuendeleza msako nafasi ya pili

INATOKA UK. 24

kwenye michezo iliyobakia na kumaliza katika nafasi ya pili," alisema Mgunda.

Aidha, alisema anafahamu Dodoma FC ni timu nzuri na wenyewe watapambana kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mchezo huo hivyo lazima wawe makini nao.

„Tulipofika sasa kwenye Ligi hakuna mchezo mwepesi, kila timu inapambana kupata ushindi kwenye michezo iliyobakia, sitarajii mchezo mwepesi na ndio maana nasema tumejiandaa vizuri na tutapambana kupata alama tatu," alisema Mgunda.

Simba inachuana na Azam kwenye kusaka nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi ambapo mpaka sasa kwenye msimamo, Azam yupo nafasi ya pili akiwa na pointi 60 akifuatiwa na Simba wenye pointi 57.

Kwa upande wake, Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope alisema wanaiheshimu Simba kwa kuwa wana wachezaji wenye uzoefu mkubwa lakini wamejipanga kupambana nao uwanjani kwa lengo la kuondoka na pointi tatu.

Alisema hawatawadharau wapinzani wao na watakazania kwenye mbinu na maandalizi yao kwa ajili ya mchezo huo muhimu.

## Gamondi: Yanga bado haijafikia malengo yake

INATOKA UK. 24

wa Afrika ingawa walitolewa katika hatua ya robo fainali, walifikia malengo waliyojiwekea kabla ya kuanza michuano hiyo mikubwa Afrika.

"Lengo letu kubwa ilikuwa kucheza hatua ya makundi, tulifanikiwa na kwenda mbali zaidi na kucheza robo fainali, ukirudi kwenye Ligi Kuu hivyo hivyo tumefanikiwa kuchukua ubingwa, ukiangalia hapo sasa tumebakisha kombe la FA ambalo nalo lilikuwa kwenye malengo yetu," alisema Gamondi.

Kwa sasa Yanga wapo kwenye maandalizi ya mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Ihefu FC (Singida Black Stars) utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Gamondi, alisema tayari wameshaanza maandalizi ya mchezo huo muhimu na kuwataka wachezaji kuweka akili na mawazo yao kwenye mchezo huo.

"Huu hauwezi kuwa mchezo mwepesi, ni mtoano, makosa kidogo yanaweza yakatugharimu na kushindwa kufikia lengo letu, nimeongea na wachezaji na tunaendelea na maandalizi ya mchezo huo," alisema Gamondi.

Alisema anatamani mechi hiyo iishe ndani ya dakika 90 za mchezo na wachezaji wake wanaweza wakafanya hivyo kama watafuata vizuri maelekezo yake kama wanavyofanyaga siku zote.

# Michezo

Ijumaa Mei 17, 2024

Nipashe


**Ten Hag asisitiza Fernandez atabaki Man U**

UKURASA 21





Mshambuliaji wa Manchester United, Rasmus Hojlund (mwenye jezi nyekundu), akipiga shuti katikati ya mabeki wa Newcastle United wakati wa mchezo wao wa Ligi Kuu ya England juzi usiku, United ilishinda mabao 3-2.
**PICHA: MTANDAO**

# GAMONDI: YANGA BADO HAIJAFIKIA MALENGO YAKE

## ●●●Asema msimu haujaisha, bado hawajachukua kombe la FA, awataka wachezaji wake ku...

**Na Saada Akida**

LICHA ya kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu huku wakiwa na michezo mitatu mkononi, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema kwake bado hawajafikia malengo yao msimu huu mpaka watakapotwaa ubingwa wa kombe la FA.

Kocha huyo amewataka wachezaji wake kukumbuka mipango yao tangu walipoanza msimu.

Gamondi amesema wanatakiwa kuendelea kupambana na kutwaa ubingwa wa kombe la FA ili kutimiza malengo waliyojiwekea tangu kuanza kwa msimu huu wa 2023/2024.



Miguel Gamondi

"Bado hatujamaliza msimu, tulikuwa na michuano mitatu, Ligi ya mabingwa, Ligi Kuu na Kombe la FA, kwangu ingawa katika mashindano mawili tumefanikiwa kufikia malengo, bado nahitaji kuona tunachukua kombe la FA," alisema Gamondi.

Kocha huyo raia wa Argentina, alisema katika michuano ya Ligi ya mabing-

INAENDELEA UK. 23

# Simba SC kuendeleza msako nafasi ya pili

**Na Faustine Feliciane**

KIKOSI cha Simba leo kitaendeleza kampeni yake ya kujaribu kusaka tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika itakapocheza na Dodoma Jiji FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Simba inapambana kumaliza ligi kwenye nafasi ya Pili ili kupata tiketi ya kushiriki michuano hiyo mikubwa Afrika kwa ngazi ya vilabu.

Leo itaumana na Dodoma FC kwenye mchezo wa 28 wa Ligi Kuu ambayo inaelekea ukingoni huku wakishuhudia watani zao Yanga wakitangaza ubingwa huku wakiwa na michezo mitatu mkononi.

Akizungumza na gazeti hili, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema mchezo huo ni muhimu kwao katika kusaka kumaliza kwenye nafasi ya pili ya ligi hiyo.

"Tumejiandaa vizuri, utakuwa mchezo mzuri na sisi lengo letu ni ushindi, kama nilivyosema huko nyuma ligi haijaisha, tunaweza tukafanya vizuri

INAENDELEA UK. 23



Juma Mgunda

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >